Utuonyeshe Baba Yatutosha

Asante, Ndugu Borders. Na tumwombe Mungu sasa kwa ajili ya haja zetu. Zifanye zijulikane kwa kuinua mkono wako, "Mungu, nikumbuke."

2 Baba yetu wa Mbinguni, sasa tumekaribia ibada ya kufunga uamsho huu mdogo, mfupi. Tunakushukuru Wewe, Baba, kwa moyo wetu wote, kwa yale uliyotutendea, kundi hili la watu. Na juu ya mioyo yetu imeandikwa, wino usiofutika wa Mungu, kwamba Yesu Kristo angali hai na anaishi daima kufanya maombezi; tunakushukuru Wewe kwa ajili ya hili.

3 Tunaomba, Baba, kwamba hakutakuwa na yeyote atakayeachwa nje, kwamba kila mtu aliye katika Uwepo wa Kiungu aweze kupokea kile ninii yao . . . walichoinulia mikono yao. Utumegee sasa Mkate wa Uzima, zaidi, Baba, tunapongojea, upate kuchochea imani yetu. Katika Jina la Yesu tunaomba. Amina.

4 Mnaweza kuketi. Daima kuna kitu kuhusu mkutano ambacho ni vigumu kuuacha. Tunapiga vita, tunapambana, tunajitahidi kote nchini, lakini basi inapofikia wakati ambapo mnaanza kufahamiana kwelikweli, mnakatiza na inabidi mwende mahali pengine. Ndugu ndio kwanza waniambie muda mfupi uliopita, yule ndugu *pale*, ninyi nyote mlinikaribisha tena; ninawashukuru kwa hilo. Hilo linaonyesha kwamba bado mnalipenda Neno. Nawashukuru sana.

5 Nami ninaenda sasa, kwenye Kisiwa cha Vancouver, nitaanzia kule Jumanne usiku, huko mahali panapoitwa Port Alberni, Alberni. Port Alberni, naamini ndivyo ilivyo, upande wa pili wa Kisiwa cha Vancouver. Niko huko Jumanne, Jumatano, na Alhamisi. Na kisha Ijumaa, Jumamosi, na Jumapili ninarudi Victoria, kwenye kisiwa hicho. Kwa hiyo endapo yeyote wa watu wako anaishi karibu na hapo, mbona, bila shaka tutafurahi kukuona. Na sina budi . . . Kesho nitakuwa ninasafiri.

6 Ndugu walijitolea kunipeleka, hapa nje, kuvua samaki. Loo, jamani. Jinsi ningependa kufanya hilo! Ninapenda hilo sana. Na Ndugu Rasmussen, mara ya mwisho nilipokuwa hapa, alinipeleka hapa Coos Bay, ama kitu kama hicho, na, loo, nikamkamata samaki mkubwa mno ambaye . . . Nilikuwa karibu . . . Ni—ningali ninaweza kuhisi mvuto huo nchani mwa ugwe, lakini ninapenda hilo sana. Lakini, mnajua, la—laiti ningeweza kufanya hivyo, halafu niketi tu kwenye mashua na kuzungumza na ndugu, na kila kitu. Ungekuwa wakati mzuri sana, nina hakika.

7 Lakini kamwe siwezi kufanya hivyo, kwa sababu hizo mashua zinazoenda huku na huko zimejaa watu, huenda

tukalazimika kungojea labda siku moja kufika huko. Nazo mashua hizo zimejaa sana, wanasema, wakati mwingine zikileta magari mia nne na zaidi kwa wakati mmoja. Mtu fulani aliniambia inakubidi kushikiwa nafasi siku moja kabla, upate kuvuka katika sehemu nyingi. Kwa hiyo, laiti ningaliweza kufanya safari hiyo, enyi ndugu. Loo, jamani. Na—na—natumaini mtaenda, nami ni—nitafurahia kwa sababu ninyi mnaifurahia, mnaona.

8 Lakini wakati mmoja, huko mbali Ng'ambo ya pili, wakati mkurupuko utakapokwisha, na kila kitu kimetulia, na... Natumaini kukutana na kila mmoja wenu. Najua wengi wenu ninyi ndugu hapa, wawindaji na wavuvi, mnajua yale maombi ya Kihindi. Wakati yote yamekwisha, natumaini, huko chini kabisa kwenye ule mburuzo mkuu wa wanyama huko chini kupitia Utukufuni, ya kwamba tutakutana tena, wakati tunahangaika kupitia huko; hiyo haina mwisho, haitakoma kamwe. Na mtu yeyote anayependa misitu na kadhalika, kama ninyi watu hapa Oregon mnavyopaswa kufanya, papa hapa katika sehemu nzuri ya ulimwengu, kuna mburuzo mkubwa wa wanyama huko ambao hauna mwisho. Nitawatafuta chini barabarani mahali fulani, nitawatafuta, lakini nitawaona huko, kwa neema ya Mungu.

9 Na dada zetu, ningewazia kumwona mtu fulani chini kwenye chemchemi, kule chini, hizo zikibubujika, niwaone dada zetu wapendwa kule chini, ambapo, wameketi chini, wakiyapapasa manyoya ya simba, ama simbamarara, ama chochote kile. Hakutakuwa na kitu cha kudhuru Kule. Unaweza kukaa hapo miaka milioni moja wala hutakuwa na muda pungufu kuliko uliokuwa nao ulipokuja hapo mara ya kwanza. Itakuwa tukufu tutakapofika Huko, ninaitamani siku hiyo. Leo ninapambana, ninajaribu, ninavuta, ninasukuma, ninalia, ninakemea, kila kitu ninachoweza kufanya, kwa sababu ninataka kuona kila mtu Huko, ninajaribu tu kwa moyo wangu wote.

10 Wafadhili wangu, jinsi ninavyowathamini watu hao, Mungu pekee ndiye anayejua jinsi ninavyowathamini. Bila shaka, wanaelewa kwamba ninajua yale ambayo wamepitia. Ninawaombea, wala si sasa tu, bali sikuzote nitawaombea. Wamepitia vita vikuu; watu ambao watafanya hivyo kuleta kitu ambacho wanaamini kuwa ni cha Mungu wapate kuwatia moyo watu wao na kanisa, ninawaheshimu. Wao pengine ni wa madhehebu mbalimbali. Labda wengine ni wa Assemblies of God, wengine Church of God, na wengine wa mashirika huru, na wengine, loo, *kitu kimoja na kingine*, lakini tuko pamoja, sisi ni ndugu.

Nina watoto wachache. Ninapoenda kuwanunulia watoto aiskrimu, nakwambia, mmoja anasema, "Niletee vanila."

Mwingine akasema, "Niletee chokoleti."

Na mwingine akasema, "Niletee stroberi."

11 Ninaporudi, ninaonekana kama nina upinde wa mvua, ninapoona rangi hizo zote mbalimbali. Lakini mnajua nini? Wote ni watoto wangu, wote wanakula aiskrimu, ladha haijalishi. Mnajua ninachomaanisha, sivyo, enyi ndugu? Ladha haijalishi, tunakula aiskrimu. Tunaamini katika Mungu yeye yule, ujuzi ule ule.

12 Nanyi mwajua, hata hivyo, upinde wa mvua ni agano. Hiyo ni kweli. Kwa hiyo tuna agano mioyoni mwetu kuwa ndugu, tukifanya kazi pamoja kwa Ufalme wa Mungu, na kwa utukufu wa Mungu. Naomba mwipeperushe bendera hiyo ya utukufu Wake muda mrefu, enyi ndugu, Mungu awe pamoja nanyi daima. Wakati saa zinapoingia giza na ni ngumu, nitakuwa nikiwaombea, nanyi mwe mkiniombea, tungali tunavua samaki, mpaka tutakapokutana Ng'ambo ya pili.

13 Maskini ndugu yetu mwenyekiti pale, niliwazia, nilipolisikia jina lake kwa mara ya kwanza, nilisema, "Hapana shaka ni Mwitaliano," nikakuta, yeye ni Mrusi. Nami nilipokuwa kule Ufini na nikiwa na mkutano, nilikuwa moja kwa moja kwenye mpaka wa Urusi. Sasa, sikilizeni, watu wanapowaambia, sio kusema hivyo kuhusu ndugu huyu mpendwa hapa, mnajua alivyo yeye, anaishi hapa pamoja nanyi, lakini kila mtu anawaambia, na tunasikia propaganda nyingi, kwamba Urusi yote ni ya komunisti. Nawe unaingia mle... Msije mkaamini upuuzi huo, kuna mamilioni ya Wakristo huko Urusi. Mbona, mnajua nini? Urusi, kuna asilimia moja tu ya Urusi, kwa ujumla, ambayo ni komunisti. Hizo ni takwimu za serikali, asilimia moja. Kile Urusi inachohitaji ni uamsho, wanahitaji watu wa Mungu kusimama na kitu kilicho halisi.

14 Wakati yule mvulana mdogo alipofufuliwa katika wafu, huko Ufini, ambalo lilitangazwa miaka miwili kabla, hapa, atafufuka katika wafu, wakati mvulana huyo mdogo alipofufuliwa katika wafu... Nao walikuwa wakinipeleka huko... huko Helsinki, tukishuka kupitia huko. Nao walikuwa na... Mimi sikuzote... Ukumbi pekee ambao niliwahi kuingia hapo awali, tangu wakati huo, ambao una alfabeti, uliketi tu yapata, nadhani, watu elfu ishirini na tano, thelathini. Nao wangeruhusu kundi moja liingie, waache niwazungumzie, kisha wanawaondoa wote, na kuingiza kundi lingine, kundi jipya ndani.

15 Nilipokuwa nikishuka kwenda nji—njiani, niliwaona maskini askari wa Kifini. Ilikuwa mara tu baada ya vita walivyokuwa navyo na Urusi, na bila shaka wangepata... watu wao wengi waliuawa. Ndipo maskini wavulana hao wadogo, baadhi yao ni wachanga sana kamwe hawanyoi, wenye uso laini, wamevaa maskini hizo buti kubwa, hivyo visu vikubwa na...

vikining'inia ubavuni mwao, wangeshuka kuja barabarani, nao wangeniweka katikati yao.

16 Nilipopitia kule chini, hao askari wa kikomunisti, sasa, sina haja ya kuchukua neno la mtu yeyote kwa hili, nilikuwa huko, askari wa kikomunisti, nilipopita, wangesimama pale, pamoja na saluti hiyo ya Kirusi, machozi yakitiririka mashavuni mwao. Wakasema, "Tutampokea Mungu kama huyo, anayeweza kuwafufua wafu." Ilienea Urusi nzima.

17 Jambo ni kwamba, kilichoifanya Urusi iwe ya kikomunisti ni kwa sababu ya udhaifu wa kanisa Katoliki huko, ambao walichukua fedha zote kutoka kwa watu wala hawakuwapa kitu badala yake, wala hawakuishi maisha yoyote tofauti na kadhalika. Hilo ndilo linalougeuza ulimwengu mzima kuwa komunisti. Hiyo ni kweli. Wanapoona kitu kilicho halisi, wako tayari kutoka, kukipokea.

18 Nilimwona askari wa kikomunisti wa Kirusi akimkumbatia askari Mkristo wa Kifini na kumpigapiga mgongoni. Sikilizeni, ndugu, chochote kitakachofanya Mrusi na Mfini kukumbatiana kitasuluhisha vita milele. Kristo ndiye jibu kwa kila tatizo, lakini ni, kwao, halina budi kuwa halisi.

19 Kamwe siusahau usiku huo, msichana mdogo wa Kifini . . . Mimi . . . Walinipeleka kwenye bweni, na kama lilivyokuwa, wala simkujua huyo mtoto mdogo. Nayo picha yake iko kwenye kitabu huko nyuma. Kwa hiyo alikuwa na mguu mmoja mfupi inchi nne au tano kuliko huo mwingine, alikuwa ametengenezewa kiatu kikubwa chini yake, alikuwa amefungiwa ga—gango *hapa*, na kamba mwishoni mwa mguu wake mbaya ilipitia begani mwake, naye alikuwa na magongo mawili. Naye alikuwa ndiyo kwanza atoke kwenye msala wa akina mama nilipokuwa nikipita, nao maskini askari hawa wa Kifini wakiingia.

20 Nilikuwa nikitoa tamshi, nikijaribu kuzungumza nao, nikiwaelekezea kidole hao Warusi pale, jinsi walivyokuwa wakiyaheshimu mambo ya Kiungu. Na kwa hiyo tulipoingia ndani, maskini mwanamke huyu, msichana mdogo, akatoka katika msala wa kina mama. Walikuwa wakisema, "Mtu asimguse."

21 Ninawapenda watoto, nami ningewachukua wote alasiri wakati ndugu walipokuwa wakifanya mikutano, na wote wangeingia, ningechukua baadhi ya hizo pesa za Kifini na kutoka huko nje, nilikuwa na kundi la watoto kote huku na huku mitaani, nikiwanunulia peremende. Na—nawapenda watoto.

22 Na kwa hiyo msichana huyu mdogo alikuwa ametoka nje, alidhani alikosea, akatoka akaja mahali nilipokuwa, ndipo akasimama, naye akainamisha kichwa chake, maskini nywele zilizochakaa, na maskini sketi zake zimechakaa. Niligundua baadaye kwamba alikuwa mtoto yatima wa Kifini; hakuwa na baba wala mama, na kwa hiyo . . . walikuwa wameuawa vitani.

23 Naye aliponiona, nilikuwa nikienda *hivi*, naye alikuwa amesimama upande *ule*, ndipo akainamisha maskini kichwa chake chini. Nami nikasimama, wale askari wawili waliokuwa nyuma yangu wakaniashiria nisonge mbele, nao walikuwa tayari wanaimba, *Amini tu*, lakini nikangojea tu, nilijua mtoto huyo alitaka kitu fulani. Naye akanitazama tena, akainua uso wake mdogo na kuangalia, nisingeweza kuzungumza lugha yake, kwa hiyo nikamnyooshea kidole, akaja pale, mahali nilipokuwa.

24 Alipoanza, jinsi ilivyombidi kutembea, angesukuma magongo haya mawili mbele, achukue maskini bega lake na kuunyanyua mguu huo na kuuweka namna *hiyo*, kisha atembee, kisha anyanyue maskini bega lake na kuusukuma nje mguu huo uliolemaa. Nilifikiri ningemwangalia tu mtoto huyo; inashangaza sana kuwatazama watoto. Nami nikamwangalia, naye akazidi kukaribia, zaidi, zaidi.

25 Nikasimama tu kimya, nao hao askari wakageuka tu kuangalia. Ndipo aliponikaribia sana, akasimama, akanitazama, kisha akainua maskini mkono wake na kunyoosha, akashika koti langu, akabusu mfuko wa koti langu, akaliachilia. Nikamtazama tu, akaangalia juu, na machozi yakisimama kwenye maskini macho yake, kisha akachukua maskini magongo yake, akajishikilia, akapanua sketi yake ndogo, ambalo ni la Kifini sana, akasema, "Kiitos." Hiyo inamaanisha, "Asante."

26 Nikamwangalia, nikawaza, "Kama ningekuwa ndiye mnafiki mkubwa kuliko wote ulimwenguni, Mungu angejibu imani ya mtoto huyo." Nikaanza kugeuka, nikamwona akienda basi, katika ono, akiondoka kwangu, mzima. Nikageuka, nikasema, "Mpenzi," naye akaendelea kusema, "Kiitos," asingeweza kusikia neno lolote nililokuwa nikisema. Nikasema, "Kipenzi, Yesu Kristo anakuponya."

Akasema, "Kiitos, kiitos," nao wakaendelea kunisukuma.

Nikasema, "Naam, siku moja atakuja kujua."

27 Baadaye, nilikuwa na mstari mkubwa sana wa maombi, magongo na kadhalika yamelundikana kila mahali, Bwana akifunua ninii...kwa watu na kuwaita kupitia kwenye kusanyiko, ndugu yangu akasema, "Umefanya ya kutosha sasa. Inatubidi, tutahubiri tena kesho." Kwa hivyo akaja kunichukua, nami nikasema, "Ita tu ninii...kadi zingine chache tu." Basi alipofanya hivyo, aliyefuata jukwaani alikuwa ni yule msichana mdogo. Alikuwa—alikuwa na magongo yake.

28 Nikamwambia Bibi Isaacson, na huenda ameketi hapa leo, nikasema, "Bibi Isaacson, sema tu ninachosema." Nikasema, "Mpenzi, huko nje ukumbini, Yesu alikuponya. Acha baadhi ya wahudumu wakuondolee hilo gango. Uone kitakachotokea."

29 Ndipo walipoenda kule, waliondoe, niliombea tu kama mtu mwingine mmoja, naye huyu hapa anakuja huku miguu yote miwili ni mizima tu awezavyo kuwa, mikono yake juu hewani,

akimtukuza Mungu. Nijuavyo mimi, maskini mtoto huyo anaishi Ufini leo, kwa sababu . . .

Watoto, watoto ni wa ajabu, sivyo? Urahisi wa imani!

30 Ninao wasichana wawili wadogo. Wanakuwa wakubwa sasa, na bado ni wasichana wangu. Nilizoea kusimulia hadithi ndogo kuhusu, wakati mmoja nilikuwa nikingojea, mama alikuwa akiningojea, nirudi nyumbani. Nilikuwa nje mkutanoni, nao maskini hao wasichana wadogo walikuwa wakingoja pamoja nami, wakiningojea, hasa, na kwa hiyo bwana mchanga akaja nao wakashikwa na usingizi, ndipo yapata saa saba mama akawalaza kitandani. Nayo ndege ilikuwa imechelewa. Basi nikaingia, nilikuwa nimechoka sana nisingeweza kupumzika, kama jana usiku, nisingeweza hata kulala kabisa, kwa hivyo nikaamka tu yapata . . . nikalala kwa yapata saa mbili, nikaamka nikaenda sebuleni, nikaketi kitini.

31 Nami sikuzote nimetoa mfano wake. Rebekah ndiye binti yangu mkubwa. Mtoto Sharon alienda nyumbani . . . pamoja na mama yake, mnajua, miaka mingi iliyopita. Lakini Rebekah ndiye wangu mkubwa, amemzidi Sara umri kwa miaka minne, naye Sara wakati huo alikuwa na umri wa miaka minne hivi . . . loo, yapata umri wa miaka miwili, nadhani, naye Becky alikuwa na umri wa takriban miaka sita. Kwa hiyo Becky, kwangu, aliwakilisha kanisa ambalo limekuwa hapa muda mrefu. Alikuwa na miguu mirefu, mwembamba, naye Sarah ni mtoto mdogo, mwenye macho ya kahawia, mnene.

32 Na kwa hiyo, sijui, nadhani watoto wenu ni kama wangu, zile za kuachiwa; ni nguo zinazotoka kwa mmoja hadi mwingine. Kwa hiyo Sarah alikuwa anavaa pajama za Becky, nazo zilikuwa kubwa sana kwake. Walikuwa na pajama hizo za miguu ya sungura, mwajua, katika siku hizo. Na kwa hiyo, zilikuwa kubwa sana kwa Sarah.

33 Kwa hiyo asubuhi hiyo, baada ya mapambazuko, mbona, muda si muda mwajua, ni—nilisikia kelele, mtu fulani akageuka huko nyuma katika chumba kingine, wale watoto, naye Rebekah akaamka, akatambua, "Baba hapana shaka yuko nyumbani," naye huyo akatoka kitandani haraka alivyoweza, hiyo ikamwamsha Sarah, Sarah akajaribu kumfuata.

34 Becky angeweza kumshinda mbio, alikuwa na miguu mirefu. Kwa hiyo akakimbia akaruka kuutagaa mguu wangu, akanikumbatia shingoni mwangu, na kuanza kupiga mayowe, "Baba, Baba." Ndipo maskini Sarah, akija na hizo pajama za Becky zenye miguu mirefu, naye alikuwa akijikwaa, naye alikuwa mfupi sana, asingeweza kuendana na Becky.

35 Kwa hiyo basi Becky akageuka, akamtazama Sarah akishuka ukumbini, naye akasema, "Sarah, dada yangu, nataka ujue jambo moja," akasema, "Nilifika hapa kwanza, nami ninaye Baba wote, wala hakuna hata chembe yake iliyokubakia."

Mnajua, kama wengine wao wanavyojaribu kutwambia, siku hizi, wanafikiri wanayo yote, mnajua. Wamekuwa hapa muda mrefu, walianza miaka mia nne ama tano iliyopita, mwajua.

36 Naye maskini Sarah, mdomo wake mdogo ukashuka chini, macho yake madogo ya hudhurungi yakainga rangi, akaanza kuondoka, akageuka. Nikatazama upande mmoja huku Becky akiwa ameegemeza kichwa chake kwangu, *hivi*, nikamwashiria *hivyo* na kulisukuma hili goti lingine nje. Huyu hapa anakuja, akalirukia moja kwa moja, alikuwa—alikuwa. . . miguu yake isingeweza kufika sakafuni, hakuwa amekaa humu muda mrefu sana, mnajua, kwa hiyo a—alikuwa anayumbayumba, nami nilihofia angeanguka, kwa hiyo nilinyosha tu mkono na kuchukua mikono yote miwili na kuiweka juu ya Sarah, naye akaegemeza maskini kichwa chake kidogo juu yangu, namna *hii*.

37 Akageuka, akazungusha hayo macho makubwa, meusi, na kumwangalia Rebekah, na kusema, "Rebekah, dada yangu, nina jambo la kukwambia," akasema, "huenda ikawa una Baba wote, lakini nataka ujue kwamba Baba anaye mimi wote."

38 Kwa hiyo—kwa hiyo nafikiri kama tukijiachilia tu, na kumwabudu Bwana, tunaweza tukayumbayumba kidogo, maadamu anaye mimi wote, hayo tu ndiyo yanayonijalisha. Kama ninaweza tu kujisalimisha kabisa ili apate kuwa na mimi wote! Huenda nisijue mambo yote ya ndani na nje, kujua jinsi ya kushindana kanuni za imani, na kadhalika namna hiyo, lakini jambo moja:

Jamaa fulani aliniambia wakati mmoja, nilitoa tamshi, naye akasema, mtu mwerevu sana, naye akasema, "Wewe huijui kabisa Biblia yako."

39 Nikasema, "Lakini namjua Mwandishi wake vizuri sana." Kwa hivyo hiyo ni. . . Kumjua Yeye ni Uzima. Je, hamfikiri hivyo? Naam, bwana. Ni—ni. . . Kama ninamjua Yeye, atanifunulia Kitabu Chake jinsi tu anavyotaka mimi nikijue.

40 Hao ndugu waliniambia, pale tu, ya kwamba mlichukua sadaka kwa ajili yangu, ninashukuru. Kwa kweli, sikuja kwa ajili ya hiyo, mimi. . . lakini ninashukuru. Sikuzote ninaomba. . . Ikiwa gharama zote zimelipiwa na kadhalika, nao wachukue sadaka, basi mnajua ninavyofanya nazo? Ninazipeleka kwenye huduma za kigeni mimi mwenyewe. Nami najua mnatoa sehemu ya riziki zenu, sasa ziko mikononi mwangu, ninawajibika sasa, zimetoka mikononi mwenu. Lakini kwa uwezo wangu wote nitazitumia kwa Ufalme wa Mungu na kwa kuujenga huo Ufalme.

41 Ninaomba kwamba itawarudia mara elfu. Mliketi katika jengo hili lenye joto, mkaufadhili mkutano, m—mkafanya kila kitu vizuri. Nawashukuru. Hakuna. . . hakuna niwezacho kufanya ila kusema hivi: "Mungu ambariki kila mmoja wenu."

Natumaini Yeye atafanya hivyo kwa yote mnayohitaji katika safari hii, nami nina hakika atawabariki.

42 Sasa, nataka kuwaulizeni swali pamoja na fadhili. Ninajiandaa kuondoka mara moja sasa. Labda ninii yangu... Nina yapata...Sina budi kwenda kwa Ndugu Leeming, wengi wenu nyote mnamfahamu, huko Florida, huko pamoja na Wafanyabiashara Wakristo, mikutano kadhaa, na halafu ninaelekea ng'ambo, ambako huwezi kuketi hivi; waganga wakisimama pale, wakikupa changamoto. Kila kitu...U—unaninii tu...Huko kwenye uwanja wa vita hapa, lakini huko uko.

43 Basi wakati kila kitu kinakuwa kigumu sana na kadhalika, je, ninaweza kuwategemea watu wangu, marafiki, huku Oregon kuniombea? Mtafanya hivyo? Niombeeni tu, nitakuwa nikiwategemea. Sikuzote nitawaombea.

44 Na kama sitawaona tena, upande huu wa mto, nitawaona Ng'ambo ya pili nikiwa na ushuhuda ule ule: "Yesu Kristo yeye yule jana, leo na hata milele." Ninaamini Yeye ni Mwana wa Mungu ambaye bado anaokoa kutoka dhambini. Aliteswa chini ya Pontio Pilato, akasulubiwa, akafa, akafufuka siku ya tatu, na yu hai daima kufanya maombezi tunapoungama; ninaamini ya kwamba Yu hai.

45 Nataka kuchukua muda huu kumshukuru m—mtu, kapteni, au jemadari, au yeyote yule, aliyeturuhusu kulitumia jengo hili zuri. Ninashukuru kwa hilo, nikitumaini ya kwamba Mungu atakibariki sana kitengo hiki, cha chochote kile, kilichoturuhusu tulitumie hili, naomba kusiwe na hata mmoja wao atayepotea, kila mmoja wao na aonekane pamoja na watakatifu wa Mungu kwenye siku hiyo, ombi langu aminifu. Asanteni, enyi waungwana, nami ninamtumainia Mungu, kwa moyo wangu wote, kwamba kila kitu kitakuwa shwari kwenu kote katika safari ya maisha.

46 Na sasa, natumaini kurudi siku moja. Mungu akipenda, ndugu zangu wakiwa tayari kufanya hivyo, kurudi kwenye hii mikutano hapa, ambapo tunaweza kuwa na mkutano mrefu. Ningependa kuwa na wakati ambapo ningeweza kuzungumza na ndugu zangu wachungaji asubuhi moja, na—na kuzungumza juu ya mambo ya Bwana.

47 Shukrani kwa mama huyu mzuri, hapa, ambaye amecheza kinanda, na mpiga piano, tunawashukuru, mabawabu wote, kila kitu; Mungu awe nanyi daima.

48 Sasa, alasiri ya leo tutamwombea kila mtu, wala sitaki kuwaweka muda mrefu, nimewaweka muda mrefu kila usiku. Ningesema, "Samahani," lakini ndugu, dada, kwa njia fulani, nikiuweka huu Ujumbe rahisi tu niwezavyo, ninajua ya kwamba hiyo Mbegu imepandwa; Itazaa katika majira Yake.

Nanyi niombeeni ninapoendelea, nami sikuzote nitakuwa nikiwaombea na kumwomba Mungu awasaidie.

49 Ninataka kusoma kifungu kimoja kutoka katika maskini Biblia hii iliyobarikiwa, alasiri ya leo, kwa ajili ya somo, sio kunena kwa muda mrefu, maana sina budi kuwaombea wagonjwa wote. Mnampenda? Semeni, "Amina." Je, mnamwamini? Semeni, "Amina." Ni wangapi waliowahi kuusikia ule wimbo mdogo wa *Amina*? Loo, hakika. Hilo ni jema. Hilo ni sawa. Ninaupenda huo, *Amina*, Ndugu Zepp huuimba vizuri sana.

50 Ninataka kusoma kutoka katika Yohana Mtakatifu mlango wa 14 na kifungu cha 8 pekee.

> *Filipo akamwambia, Bwana, utuonyeshe Baba, yatutosha.*

Labda nitasoma kifungu kinachofuata:

> *Yesu akamwambia, Mimi nimekuwapo pamoja nanyi siku hizi zote, na bado. . .wewe* hunijui, *Filipo? aliyeniona mimi amemwona Baba; basi wewe wasemaje. . ., Utuonyeshe Baba?*

51 Ningependa kuchukua somo hili: *Utuonyeshe Baba Yatutosha*. Kwa maneno mengine, inamaanisha "inaridhisha." "Ukinionyesha Baba, itaturidhisha."

52 Sasa, hicho kimekuwa ndicho kilio cha moyo wa mwanadamu katika nyakati zote, ni kumwona Mungu. Ayubu wa kale alilia, "Laiti. . ." katika dhiki yake, "Laiti ningejua alikoishi! Laiti ningeweza kwenda kubisha mlangoni Pake na kuzungumza Naye!" Kila mtu ametaka kumjua Mungu na kumwona Mungu. Ayubu alitaka kumwona. Musa alitaka kujua ni Nani huyo aliyekuwa kwenye kile kijiti kilichowaka moto, chi-. . .kisha akasema, "Nionyeshe utukufu Wako." Alitaka kuona dhihirisho fulani apate kujua kwamba alikuwa ni Mungu. Na sisi sote tunafanya hivyo, sote tunatamani kuona kitu ambacho ni halisi, ninii. . .kitu cha kuthibitisha kwamba Mungu yuko.

53 Na ni kwa njia yangu nyenyekevu ya kuwazia kwamba inampendeza Baba kujionyesha Mwenyewe, kujidhihirisha Mwenyewe; Yeye anawapenda watoto Wake. Jinsi ninavyopenda kuwaambia watoto wangu jambo fulani na kutoa sharti, halafu niwaone hao watoto wakitekeleza hayo, nami ninaweza kuwaonyesha jambo fulani zuri.

54 Jinsi ninavyomwambia mvulana wangu mdogo, Joseph, "Iwapo utakuwa tu mvulana mzuri sasa, na—na kumjali Mama, unajua, Jumamosi nitakaporudi, nitakupeleka kuvua samaki."

Na kumwona mvulana huyo mdogo, mama yake akisema, "Alikuwa mtiifu tu, Bill, kama awezavyo kuwa juma hili."

55 Jinsi nilivyo na furaha kwenda kumwonyesha mvulana huyo mdogo, kumpeleka akavue samaki, ninapenda kumwonyesha kwamba ninataka kuwa mwema kwake, kwa sababu yeye ni sehemu yangu. Nataka—nataka awe kama ninavyotaka kuwa, Mkristo. Nami napenda kudhihirisha kile ninachomtaka awe, kupitia kwangu.

56 Naye Mungu anataka kujidhihirisha kwa watoto Wake, lakini anaomba sharti moja tu: "Kama utaamini." Hayo tu ndiyo anayoomba, anatoa Neno Lake na kukuuliza kama utaliamini.

57 Sasa, nitazungumza. . . Sasa bado, si ilikuwa ajabu, hapa, kwamba Filipo, yule shujaa mkuu ambaye alikuwa ameona kazi hizo kuu sana za Kristo, akaenda akamchukua Nathanaeli na kumleta kule, mahali hapo, na kuona madhihirisho ya thibitisho la Maandiko ya kwamba Yeye alikuwa ndiye Masihi, kisha akasema, "Sasa, Wewe utuonyeshe Baba yatutosha"?

58 Sasa, je, mliona ki—kifungu kinachofuata, kifungu cha 9? Kasema, "Mimi nimekuwapo pamoja nanyi siku hizi zote, Filipo, nawe hunijui?" Jinsi ninavyowazia hiyo ingekuwa kwetu, alasiri ya leo, kwamba Mungu katika rehema Zake amejidhihirisha Mwenyewe mara nyingi sana kwetu, na hata hivyo hatutambui.

59 Sasa, nitazungumza juu ya "Njia Nne Za Kumwona Mungu." Sasa, watu wengi hujaribu kumweka mbali kama tukio la kihistoria, lakini hebu tumwangalie tu Mungu katika njia nne. Nami nafikiri kwamba ikiwa Mungu anaweza kuonyeshwa vizuri, bila shaka lolote, ya kwamba Mungu, kwa njia nne mbalimbali, amesimama papa hapa, alasiri ya leo, hilo linapaswa kusadikisha, sivyo? "Njia Nne Za Kumwona Mungu." Nitazungumza juu ya "Mungu Katika Ulimwengu Wake," "Mungu Katika Neno Lake," "Mungu Katika Mwanawe," na "Mungu Katika Watu Wake." Na sasa, ningeweza kuchukua dazani moja zaidi, lakini nataka kutulia kwenye mambo hayo manne, kwa dakika thelathini zijazo, Mungu akipenda.

60 Hebu tuchukue ya kwanza sasa, "Mungu Katika Ulimwengu Wake." Ni nani aliyeiumba dunia? Tunaambiwa kwamba inasimama angani. Inawezaje kuzunguka kikamilifu sana, kikamilifu kuliko chombo chochote?

61 Nimevaa saa ya dola mia tatu ambayo nilipewa na Dk. Guggenbuhl nchini Uswisi. Alinipa kwa sababu ina kengele, kwa ajili ya mahojiano na kadhalika. Na ni Vulcain Cricket, mojawapo ya zile bora sana ambazo Uswisi hutengeneza, lakini hata hivyo, itapoteza wakati, itaongeza wakati, si kamilifu. Kitu chochote atengenezacho mwanadamu si kikamilifu, lakini yote Mungu afanyayo ni makamilifu. Mnaona?

62 Angalieni, jinsi anavyoweza kuifanya dunia hii ilizunguke tu, jua kikamilifu daima, ikienda mbio, mwaka baada ya mwaka, siku baada ya siku, ikizunguka ikweta, kuzunguka, mzingo wake, na kila kitu, na kuzifanya hizo nyota na kadhalika, mpaka

wanaweza kubashiri kupatwa kwa mwezi miaka ishirini kufikia dakika moja. Kamilifu kabisa!

63 Basi ni nini kinachoishikilia huko juu? Juu ni wapi na chini ni wapi? Tunajuaje? Wale walio kwenye Ncha ya Kusini ni, kwetu sisi, wanaangalia *huko*, wakisema ni juu; nasi kwenye Ncha ya Kaskazini tunaangalia *huku*, na huko ni chini hadi Ncha ya Kusini. Ni gani sahihi?

64 Jinsi inavyoelea kikamilifu! Zungusha kitu chochote angani uone kama kitasimama pale mizunguko miwili bila kuondoka kwenye mzingo wake. Lakini Mungu, kikamilifu, anaishikilia dunia yote katika udhibiti Wake. Tunaamini jambo hilo, ya kwamba Mungu hufanya hivyo. Hakuna nguvu nyingine, hakuna kitu kingine kingeweza kufanya hivyo ila Mungu, Mungu peke yake.

65 Na je, uliwahi kwenda huku nje baharini, uone bahari hiyo kubwa yenye hasira, hayo mawimbi makubwa meupe yakipiga mle ndani, yamekasirika? Mnajua, karibu sehemu nne kwa tano ya dunia imefunikwa na maji, na wakati mmoja yaliifunika dunia nzima. Jinsi yangetaka kupita pale kama yangeweza, lakini mnaona, yatafika tu *umbali huu*. Kwa nini? Mungu ana mlinzi anayeyachunga, huyo ni mwezi.

66 Mwezi unadhibiti, Mungu aliuweka pale kuidhibiti bahari. Kama mwezi huo ungewahi kusonga inchi chache kutoka kwenye mzingo wake, dunia yote ingefunikwa na maji, katika muda mfupi tu. Tazama anapogeuza kichwa chake kuona upande wa pili wa dunia una nini, jioni wakati, au, asubuhi, na kadhalika, jinsi mawimbi yanavyotanda, na hapa yanaingia tena kwa hasira, lakini mlinzi pale anasema, "*Hiyo* ndiyo mipaka yako; kaa papo *hapo*." Na hata hivyo kuna maji ya kutosha huko nje, pamoja na kupinda kwa dunia, kukifagilia mbali kitu hicho kote; lakini Mungu ana udhibiti. Amina. Loo, "Jinsi Wewe ulivyo mkuu, jinsi Wewe ulivyo mkuu!" Jinsi anavyofanya jambo hilo, jinsi Yeye. . . Ni zaidi ya uwezo wetu. Jinsi tungeweza kutumia saa nyingi kwenye hilo!

67 Hebu tushuke kwenye jambo lingine. Hebu tuangalie maua, jinsi yanavyoishi, kufa, kufufuka tena. Jinsi ambavyo ungeweza kuchukua nyasi zako wakati wa kipupwe, na kumwaga bamba la zege juu yake. Ni wapi pana nyasi nyingi zaidi kwenye msimu ujao wa kiangazi? Papo hapo karibu na ukingo wa njia. Ni kwa nini? Ni ule uhai ambao. . . ulificha chini ya hilo zege. Lakini wakati huyo mdhibiti uhai wa mimea, jua, j-u-a, linapoanza kuangaza, huwezi kuuficha uhai huo. Utajitokeza moja kwa moja, na kupenya utoke nje, na kukiinua kichwa chake moja kwa moja juu, kwa utukufu wa Mungu. Hiyo ni kweli?

68 Huwezi kuuficha uhai. Haidhuru. . . Unaweza ukazikwa baharini, unaweza. . . popote ulipo, utaitika kwa vyovyote vile, M-w-a-n-a atakapokuja, Mwana wa Mungu, Uzima wote wa

Milele utafufuka pamoja Naye, maana Yeye ana Uzima wa Milele, naye huwapa wale atakao.

69 Na sasa angalia jinsi Mungu aishivyo katika ua, jinsi aishivyo katika majani ya mti, jinsi yatakavyopukutika, kwenda chini, utomvu utashuka, kwenye mzizi, Akili fulani ikiudhibiti, unashuka kwenye mzizi kujificha wakati wote wa kipupwe, unarudi tena katika majira ya kuchipua, ukizaa tunda, na kadhalika. Je, unafanyaje hilo? Umepita ufahamu wangu. Nini . . . Hapana shaka kuna Akili fulani, mahali fulani, inayoudhibiti; hauwezi kufanya hivyo wenyewe.

70 Hakuna kitu kitakachouambia mpichi huo, *huko* nje, au, huo mpea, "Aisee, majira ya kipupwe yanakuja," yapata katikati ya Agosti, "ninyi majani yote, tokeni hapo upesi sana. Ewe uhai, teremka chini kwenye mizizi upesi ukajifiche, usipojificha, utakufa." Haujui kufanya hivyo wenyewe. Ni Akili fulani inayoudhibiti, Akili ya juu kabisa iliyopo, Mungu.

71 Vema, kama Mungu anaweza kuliambia jani, uhai wa jani hilo kuliondokea na kushuka mle na kukaa, au uhai utoke sehemu ya juu ya huo mti na kuingia mizizini, je, hawezi kufichua siri za mioyo ya watu kwa watumishi Wake? akili ya Mungu? Mbona, kitu hicho chote kimeundwa na akili, Mungu ndiye Akili ya juu kuliko zote.

Waangalie mabata, wa—wanyama, jinsi wote wanavyodhibitiwa na Mungu.

72 Hivi majuzi, mimi na mwanangu tulikuwa Bombay mkutanoni. Ndipo tulipofika huko, nilikuwa nikisoma gazeti, ni nchi yenye lugha mbili, na kwa hivyo liliandikwa kwa Kiingereza, nalo lilisema, "Nadhani matetemeko ya ardhi yamekwisha."

73 Siku chache kabla ya hapo . . . Mwajua, India si kama nchi yetu. Tuna nyua nzuri zilizofumwa, wao huokota mawe na kutengeneza nyua zao, na wanajenga minara yao na kadhalika. Kuna joto sana, karibu na ma—maeneo ya huko, mwajua, na ikweta. Kwa hiyo ko—kondoo na ng'ombe, alasiri, wanakuja na kusimama kuzunguka kuta hizi, nao wanaingia kwenye ki—kivuli, nao maskini ndege wanajenga viota vyao kwenye hizo kuta.

74 Basi siku moja jambo fulani lilitukia, maskini ndege wote waliruka wakaondoka, hakuna aliyejua ni kwa nini, wakaziondokea hizo kuta, wakatoka, hawakujua walikoenda, wakaketi kwenye miti mahali fulani. Wasingerudi kwenye kiota chao, wala ng'ombe hawangeingia.

75 Kila mtu alisema, "Kwani kuna nini?" Hao ng'ombe, hao kondoo, wamesimama huko nje, wameegemeana katika hilo jua kali, huko nje kabisa katikati ya uwanja, wasingeingia; walishangaa ni kwa nini.

76 Tena kesho yake, wakafanya vile vile, na siku ya tatu wakafanya vivyo hivyo. Ndipo tetemeko la ardhi likatikisa mahali pale vipande vipande, hizo kuta zikaanguka. Hao ng'ombe na kondoo wangalikuwa wamesimama kule chini, wangalikufa, maskini ndege hao wangepondwapondwa. Kesho yake hakuna kilichotokea, ndipo basi siku ya tano, basi maskini hao ndege na kadhalika wakaanza kurudi tena; tetemeko la ardhi lilikuwa limekwisha.

77 Hivi hamwoni, ni Mungu yeye yule ambaye angeweza kuwaongoza kwenye safina, katika siku za Nuhu, ni Mungu yeye yule anayeweza kuwaondoa hatarini. Naam, ikiwa Mungu, kwa silika anayompa ndege kujua kuzitoroka kuta zinazoanguka, ni zaidi sana vipi tunapaswa kuzikimbia kuta hizi kubwa, ndefu za kikanisa, ambazo hazina budi kubomoka kwa uvuvio wa Roho Mtakatifu! Ondokeni, mwendeeni Mungu upesi. Usiweke jina lako kwenye kitabu, zaliwa mara ya pili, ujazwe na Roho Mtakatifu.

Mungu katika maumbile. Mungu alimpa maskini ndege huyo asili; anaiamini, a—anaitumaini.

78 Hapa, si muda mrefu uliopita, nilikuwa kule juu Canada, na kulikuwa na hao mabata kule juu, kule juu kwenye dimbwi, na jinsi hao, wakizungukazunguka kwenye dimbwi. Watakuwepo sasa. Katika yapata, Bwana akipenda, katika yapata mwezi mwingine mmoja nitaenda kwenye safari ya kuwinda huko. Maskini hao. . . Mabata wanatoka kusini, huko chini kabisa Louisiana, Alabama, Texas, mashamba ya mpunga, nao wanaruka hadi Canada, nao wanazaa maskini vifaranga wao huko juu kwenye hayo mabwawa, vinamasi, ama—ama maziwa.

79 Sasa, huyu hapa maskini bata dume, alizaliwa papo hapo kwenye ziwa hilo, alizaliwa msimu huo wa kuchipua, hajawahi kutoka kwenye dimbwi hilo, hilo tu ndilo ajualo, amezaliwa mumo humo. Lakini usiku mmoja kutakuja wi—wimbi jeupe mlimani kule juu, kutakuwa na theluji itakayoupiga mlima huo, upepo huo baridi utashuka kupitia hilo bonde.

80 Maskini bata huyo dume ataenda moja kwa moja katikati ya dimbwi hilo, achomoze maskini mdomo huo hewani, na kulia mara nne ama tano, na kila bata humo dimbwini atamjia moja kwa moja. Kwa nini? Atainuka moja kwa moja kutoka kwenye dimbwi hilo na kuondoka, bila dira wala chochote kile, moja kwa moja tu hadi Texas awezavyo kwenda, kwenye hayo mashamba ya mpunga. Kama akikaa muda mrefu zaidi, kutaganda, watakufa.

81 Hajawahi kutoka humo. Anajuaje pa kwenda? Anaitumainia ile silika aliyopewa na Mungu. Na ikiwa bata ana akili ya kutosha kuiondokea hatari na baridi, ni zaidi sana vipi Kanisa linapaswa, kwa uwezo wa Roho Mtakatifu na ufufuo

wa Kristo, kuiondokea kanuni ya imani inayokufa! Mnaona ninalomaanisha? Silika.

Wakati mmoja nilikuwa nikilima, mimi na baba, farasi wakaendelea kukoroma, nikasema, "Baba, kuna nini? Kwani kuna mbwa mwitu huko nyuma?"

Akasema, "La, mwanangu, dhoruba inakuja."

Nikasema, "Ati dhoruba?" Nilikuwa nikiendesha kaltiveta ya kale, wengi wenu mnajua hizo ni nini, kasema, "Ati dhoruba?" Nikasema, "Bila wingu mahali popote?"

82 Akasema . . . Akasimama, kamwe sitamsahau maskini jamaa huyo mzee, akatoa leso yake nyekundu, na kupangusa jasho usoni mwake, akasema, "Billy, una mengi ya kujifunza, Mwanangu." Akasema, "Unaona, Mwenyezi amempa farasi huyo silika apate kwenda mahali pa salama." Kasema, "Kuna dhoruba inayokuja, mahali fulani, nao wanaweza kunusa dhoruba hiyo."

83 Nikawazia, "Baba, mimi . . . " Nikasema, "Vema." Wala sikuwa nimelima raundi mbili zaidi hadi ilikuwa vigumu kumtoa hu—huyo farasi upesi vya kutosha, radi, ngurumo, na kila kitu, na hii hapa dhoruba. Waliishika kabla haijafika huko.

84 Na kama Mungu anaweza kumpa farasi (Nena kuhusu hisia za farasi!), anaweza kumpa farasi silika na akili ya kutosha kujua jinsi ya kujikinga na hatari, ni zaidi sana vipi sisi tunavyopaswa, kwa uvuvio wa Roho Mtakatifu, kukimbilia usalama tunapoona wakati kama huu ukija! Naam. "Utuonyeshe Baba, yatutosha." Loo, jamani, jinsi ningeweza kukaa kwenye hilo!

85 Hebu mchukue nguruwe mzee wa kike, naye ana makapi yake upande wa kaskazini mwa kilima, nawe usome matangazo, uh, mtangazaji wa habari, kwenye redio au gazetini, anasema, "Kesho itakuwa siku nzuri, kavu," maskini nguruwe huyo mzee ayachukue makapi hayo kutoka upande huo wa kaskazini mwa kilima, ayapeleke upande wa kusini wa kilima, wewe angalia, anajua zaidi kulihusu kuliko magazeti yote na matangazo ulimwenguni, angalia baridi ikiingia.

86 Hebu angalia unapoenda kuwinda sungura, na kuwaona wakirudi nyuma kabisa chini ya mafungu ya vichaka, na vitu kama hivyo, na kujitafutia maficho, na kuketi huko nyuma kwenye mashimo, naye mtangazaji anasema, "Itakuwa hali nzuri ya hewa," kamwe usiamini hilo. Sungura huyo anajua zaidi juu yake kuliko jamaa hao wote wakiwekwa pamoja. Anatumainia silika aliyopewa na Mungu, ni Mungu akiandaa njia kwa ajili ya viumbe Vyake. Na ni zaidi sana vipi uumbaji wa mwanadamu ulivyo wa juu zaidi kuliko uumbaji wa mnyama! Ni zaidi sana vipi Roho Mtakatifu alivyo kwa Kanisa, kuliko vile silika ingekuwa kwa bata, ama farasi, ama chochote kile! Ningeweza kuchukua saa mbili juu yake.

87 Jambo moja zaidi ningependa kulifikia. Hapo ndipo nilipompata Mungu kwa mara ya kwanza, hiyo ilikuwa Biblia yangu ya kwanza, kuona ilibidi kuwe na Kitu kinachofanya mambo haya. Mungu yuko katika ulimwengu Wake. Jinsi ninavyopenda machweo ya jua, kusimama na kulitazama jua likitua na kulia, kulitazama likichomoza, na kulia; ninalipenda.

88 Nilitoa tamshi, jana usiku, kuhusu kuwa mwindaji. Napenda kuwinda, nimewinda tangu nilipokuwa mvulana mdogo. Nimewinda ulimwenguni kote: Afrika, India, na kila mahali. Wengi wenu mnamfahamu Bud Branham katika Rainy Pass Lodge huko Anchorage, Alaska, ndege kumi na sita zinazoingia, huyo ni binamu yangu. Tumetoka katika ukoo wa wawindaji na tunakupenda, kuko moja kwa moja ndani yetu; tunapenda kuwinda.

89 Nami nilikuwa nikienda hadi Colorado, ambako nilichunga ng'ombe kule juu, kwa muda mrefu, kwenye ranchi. Na huko, kuwaingiza na kuwatoa makundi, Bw. Jeverez . . . Huenda ameketi papa hapa alasiri ya leo, anaishi tu papa hapa Idaho sasa.

90 Na kwa hiyo mimi na yeye tulikuwa tukipanda kule pamoja na kuwinda, kuwinda kulungu; ninapenda kuwawinda. Tulikuwa na kama themanini katika kundi kule nyuma, tulichukua tu kile . . . mmoja kila mwaka, yale tuliyohitaji, nalo kundi hilo likazidi kuwa kubwa. Kwa hiyo basi, Bw. Jeverez, mtu wa mwituni kwelikweli, alijua kuwinda, alijua yote ndani na nje.

91 Ningesaidia kuwapa ng'ombe chumvi, na kuwaingiza mle ndani, na kuwakusanya, na kadhalika. Nilijua kila pembe huko nyuma kwenye Continental Divide, kufikia karibu na mahali unapovuka Mpito wa Berthoud, unashuka chini, kisha unapitia Mpito wa Rabbit Ear. Continental Divide inakuja katika mandhari, Mto Troublesome humwaga maji yake chini *huku*, nalo Shirika la Hereford hulishia kwenye bonde *hili*, na kuna mikondo ya mashariki na magharibi.

92 Tungepanda kwenye mkondo wa mashariki, tuwafungie farasi wetu, kisha tutengane, na kushuka kwenye mkondo wa magharibi, umbali wa maili na maili na maili, labda tusionane kwa siku kadhaa, tukiwinda.

93 Mwaka mmoja nilikuwa huko juu nikiwinda. Ningepanda huko juu, juu sana niwezavyo kupanda, niketi pale jioni, jua linapotua. Na, loo, jamani, nena kuhusu Mungu! Nilikuwa huko juu siku moja, kulikuwa kukavu, kulungu walikuwa hawajashuka bado, hakuna theluji ya kutosha na kadhalika kuwaleta chini. Wao ni wanyama wa mwituni, wanakaa huko juu, kwa sababu hawataki kushuka kwenye ustaarabu. Inahitaji theluji na kadhalika kuwatelemsha chini wakati mwingine.

94 Ndipo wakati. . .Nilikuwa huko juu nikitembea huku na huko, nikitazama, nami nikamfungia farasi wangu huko chini sana asubuhi hiyo, nikaenda hadi kwenye mpaka wa msitu huo, nikifanya mzunguko mkubwa, nikishuka kwenye kile tunachokiita Genge Potevu, na kushuka kupitia njia hiyo. Hakuna mgeni anayeingia huko, mbona, ni mbali sana kwake.

95 Kwa hiyo huko nyuma kabisa, nilikuwa nikitembea, nami nilikuwa na bunduki yangu, na nilikuwa nikitembea pale, ndipo ikatokea dho—dhoruba. Mnajua jinsi ilivyo huko juu kabisa milimani, dhoruba itatokea, kisha theluji, halafu inayeyuka, nao upepo utavuma, na jua litawaka. Hali ya hewa ya kila namna katika Oktoba huko juu, inabadilika wakati wote. Kwa hivyo hakukuwa kumekuwako na theluji ya kutosha kuwashusha chini, kwa hiyo nilikuwa karibu na mpaka wa msitu.

96 Nami nikaingia mahali pa wazi, ambapo kimbunga kilikuwa kimeisokota miti na kuipeperusha pamoja. Nami nilikuwa nikipanda kupitia huku, ndipo ikatokea dhoruba kubwa, nzito, ikinyesha, nami nikarudi nyuma ya mti, nikasimama namna *hii*, nyuma ya mti, mpaka dhoruba ilipokwisha. Nami nilikuwa nimesimama pale, karibu nishikwe na usingizi. Pepo zikivuma na kadhalika, nawe ungeweza kumsikia Mungu akinena kupitia mngurumo wa hiyo misonobari. Nikawazia, "Ee Mungu, jinsi Wewe ulivyo mkuu!" Ndipo baada ya dhoruba kwisha, nilisimama pale kidogo, kidogo *nasinzia*, Nusura nianguke mara mbili au tatu, nikalowa maji kidogo.

97 Kwa hiyo mimi. . .Ulikuwa mvumo mkali sana nami nikafuatilia nyuma, nikawazia, "Utukufu kwa Mungu. Ni ajabu jinsi gani kuwa huku juu, kuwa peke yako pamoja na Mungu, siku mbili sasa sikuwa nimemwona mtu yeyote hapa." Kwa hiyo. . .Mia. . .Uko maili arobaini kwa vyovyote vile kutoka kwa njia ya reli. Uko mbali sana na magari, hakuna petroli, sigara, takataka zote zinazovunda za kile kiitwacho ustaarabu. Nikawazia, "Ni ajabu sana kusimama hapa."

98 Nikatazama jua likitua, huku, Oregon, ng'ambo huko, na hapo jicho Lake kubwa mno, la kupendeza likichungulia kule, nami nikawazia, "Hiyo ni kweli. Jicho Lake liko juu ya shomoro, nami ninajua Yeye ananiangalia." Unaweza kumwona Mungu mahali popote, ikiwa utaangalia tu pande zote, amekuzingira kote, kila mahali; Yeye yuko katika maua, maumbile, kila mahali. Nilimwona pale.

99 Ndipo ikawa nilitazama, nami nikamsikia maskini mbwa mwitu akipiga kelele juu ya kilima pale, mwenzake akamjibu huko chini kabisa. Sasa, nena kuhusu kilindi kikiita kilindi, sikia mlio huo wa mbwa mwitu au mbwa mwitu wa mwituni, huo unaiwasha tu moto roho yangu. Ninamsikia pale, akipiga kelele, alikuwa amempoteza mwenziwe, naye akamjibu, huko chini kabisa.

Nami nikawazia, "Ee Mungu, nina Mwenza pia; nitaita Naye atanijibu siku moja." Nilisimama pale nikawaza, "Mungu, Wewe huyo hapo."

100 Nikasikia tarumbeta hapa, lile kundi la kulungu nililokuwa najaribu kulifikia. Mzee mkubwa wa kiume akatoa mlio huo mrefu, tarumbeta, namna hiyo. Kile. . . Dhoruba ilikuwa imemtenganisha yule kulungu huko juu sana, alikuwa amepoteza kundi lake, naye alikuwa akiwaita. Nikawaza, "Ee Mungu, unaishi hapa juu, hiyo ni kweli, Wewe huyu hapa." Huyo *hapo* katika hilo kundi la kulungu, Huyo *hapo* katika mwito wa huyo mbwa mwitu.

101 Ndipo ikawa niliangalia, na mahali jua lilipotokea, nayo miti isiyokauka ilikuwa imeganda, upepo huo baridi, kulikuwa na upinde wa mvua kwenye hilo genge, nikasema, "Huyo hapo kwenye upinde wa mvua. Amina. Huyo hapo. Hilo hapo lile agano, kamwe hatauangamiza tena kwa maji, aliahidi."

102 Nao upinde wa mvua pia ni, Ufunuo 1, ambapo juu ya Mwana wa Mungu, na juu ya Kanisa, vile vinara saba vya taa vya dhahabu, ulikuwa ni upinde wa mvua. "Alionekana mithili ya jiwe la yaspi na akiki. Wa Kwanza na wa Mwisho. Yeye aliyekuwako, aliyeko na atakayekuja." Loo jamani, jamani! Kila mahali unapoangalia, unaweza kumwona Mungu kama tu utayafungua macho yako. Angalia pande zote, Yeye yuko kila mahali.

103 Nilikuwa nimesimama pale, na kwa ghafla maskini kuchakulo mdogo wa misonobari. . . Ni wangapi wenu watu wa Oregon mnajua wao ni nini? Yeye ni polisi wa misituni mwenye koti la bluu, lakini kelele tupu wala hamna kuchakulo. Aliruka pale na kulia, "Kwe, kwe, kwe, kwe. Kwe, kwe, kwe, kwe."

104 Nami nikawazia, "Kwani una shida gani, jamaa mdogo? Sitakudhuru." Kwa hiyo basi upinde wa mvua niliutazama tena, nikasema, "Utukufu kwa Mungu," na nikauzunguka tena na tena mti huo mbio kadri nilivyoweza kwenda, nikipaza sauti, naye akanitazama tu, huku tu ni "Kwe, kwe, kwe."

105 Nikawaza. "Kwani nilikusisimua? Ninamwabudu Muumba wako. Hupendi hayo? Hebu nikuonyeshe jinsi inavyofanywa tena," nami huyo nikauzunguka huo mti tena. Kama. . . Wangefikiri walikuwa na mtu huko nje ametoka kwenye hospitali ya wendawazimu, nadhani, kama mtu alikuwa. . . Sikujali, nilikuwa nikimwabudu Mungu. Nilimwona, nilimsikia kila mahali. Unaweza kumwona kama ukiangalia tu huku na huku, Yeye ni halisi.

106 Nami niliuzunguka na kuuzunguka mti huo mbio sana nilivyoweza kwenda, huku nikimsifu Mungu, na kutupa mikono yangu juu, na kupiga mayowe, "Haleluya!" nikikanyaga chini kwa vishindo kuuzunguka huo mti tena na tena, kama

mwendawazimu, lakini nilikuwa na. . . nikijifurahisha sana, nilikuwa na wakati mzuri.

107 Nikawazia, "'Loo, ni vizuri kuwa hapa, Hebu tujenge vibanda vitatu.' Hebu tukae tu hapa juu, mahali pazuri pa kuwa Mbele za Mungu, katika ulimwengu Wake." Kumwangalia katika ulimwengu Wake, machweo Yake ya jua, upinde Wake wa mvua, wito wa kulungu, hapa, kila mahali, Mungu yupo.

108 Nami niliwazia, "Ewe maskini kimbelembele, kwa nini umenikatisha kumwabudu Mungu wangu?" Ninamwona ameketi kwenye kisiki hiki, ambapo. . . mahali ambapo mti ulikuwa umeanguka, akifanya, "Kwe, kwe, kwe," maskini mkia umekunjwa chini yake namna hiyo, "Kwe, kwe, kwe, kwe."

109 Nikawazia, "Una shida gani? U—unadhani mimi ninatenda kigeni?" Lakini yeye, nilimwona, alikuwa ameinamisha maskini kichwa chake chini, macho yake yametokeza, akiangalia kwenye kichaka hicho.

110 Hakuwa akinipigia kelele hata kidogo, upepo ulikuwa umempeperusha tai mle ndani, mmoja. . . maskini tai wakubwa wa kahawia huko Colorado. Naye alikuwa. . . Huyo tai angemnyakua mwajua, kwa hiyo a—alimwogopa huyo tai, hakuwa. . . hakunijali mimi, lakini alimwogopa huyo tai.

111 Tai huyo mkubwa akaruka juu pale, nami nikawazia, "Jamani! Sasa, ninakuona huko nje, Mungu, Ninakuona, nakusikia huko chini katika kusikia wito huo, ninakuona kila mahali, ninakuona angani, ninakuona katika upinde wa mvua, ninakuona kila mahali. Lakini sasa, sijui kama ungeweza kuwa katika tai yule?" Kwa nini Yeye akaikatiza ibada yangu?

112 Nami nikamwangalia yule tai kwa muda kidogo. Nikawaza. . . Sasa, niliona macho yake makubwa ya kijivu yakinitazama, naye akamwangalia maskini yule kuchakulo mzee wa misonobari, kisha akaniangalia. Na nilipendezwa naye kwa sababu alikuwa jasiri, hakuogopa. Namchukia mwoga. Ninachukia mtu. . . sio kumchukia huyo mtu, lakini ule mtazamo kwamba wanaweza kusimama kanisani na kupaza sauti kama wengine na kutoka nje na wakati shindano halisi linapokuja, unaona aibu kusema wewe ni Mpentekoste, unaona aibu kukiri kuwa umeponywa kwa uponyaji wa Kiungu.

113 Loo! Mungu hawezi kutumia kitu kama hicho, anataka askari, anataka mtu fulani, anayeweza kusema kama Paulo, "Kwa njia ambayo waiita uzushi, hivyo ndivyo ninavyomwabudu Mungu wa Baba zetu." Anataka askari, uti wa mgongo, si uti wa mgongo wa kuku; anataka mtu jasiri vya kutosha na roho wa kutosha kusimama.

114 Nikasema, "Naam, ninamwona Mungu katika tai huyo, haogopi, hana woga hata kidogo." Nikawaza, "Nitaona tu jinsi alivyo mwoga." Nikasema, "Aisee, jamani, hivi unajua ningeweza kukupiga risasi?" Sauti yangu iliposikika,

alinitazama kwa makini kabisa na kuyakodoa hayo macho makubwa.

115 Nikaanza kumwona akihisi hayo manyoya, mwajua, kwa ninii yake. . . kuyanyoosha, nikawazia, "Haya basi. Haya basi. Mungu alimpa mabawa mawili apate kuepuka shida, kuepuka hatari, naye anayatumainia mabawa hayo, njia yake aliyopewa na Mungu ya kuepukia." Anajisikia kwamba mabawa hayo yalikuwa katika hali nzuri. Vema.

116 Mtu mmoja aliniambia wakati mmoja, "Ndugu Branham, huogopi kwamba utafanya makosa huko juu? Huogopi kitu fulani kitatokea huko juu?" Loo, la, maadamu kila kitu kiko katika mpangilio, mnaona, yote ni sawa. Usijali, Yeye Ndiye aliyetoa ahadi.

117 Maskini tai huyu, akiyapurukusha mabawa yake, akiyavuruga juu chini namna *hiyo*, nikawaza, "Loo, naam, haya basi." Ndipo nikanyoosha mkono kuinyakua bunduki yangu, akaruka, na kuniangalia namna *hiyo*, na kunikazia jicho lake moja kwa moja. Sasa, alijua, kwa uwezo wake, kwamba angeweza kuchukua mabawa hayo na kuingia katika msitu huo kabla sijamtupia macho. Alijua hilo, naye aliyaamini, kwa hiyo hakuogopa.

118 Kwa nini tuogope? Haijalishi ni nini kijacho. Mungu alitupa Roho Mtakatifu, "Tazama, niko pamoja nanyi sikuzote, hata ukamilifu wa dahari." Tunaogopa nini? Mungu alikuita kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, akaweka jina lako kwenye Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo. Mwana-Kondoo alichinjwa kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, jina lako liliwekwa kwenye Kitabu kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, Biblia ilisema hivyo.

119 Biblia ilisema mpinga-Kristo, katika siku za mwisho, atawadanganya wote wakaao juu ya nchi, ambao majina yao hayakuandikwa katika Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu, sio uamsho uliopita, bali msingi wa ulimwengu. Haya basi. Kwa hiyo unajua unaishi juu, uko katika jambo fulani, umempokea Roho Mtakatifu. Unaogopa nini? Amina. Mungu katika ulimwengu Wake; ninaamini hilo, nanyi je?

120 Nilimtazama jamaa huyo hapo kwa dakika chache, maskini kuchakulo huyo aliyeketi pale, akifanya, ama maskini kucha-. . . Hivyo ndivyo tunavyowaita, nyumbani, wao ni wadogo, kwa kweli, kuchakulo mdogo wa misonobari alikuwa akifanya, "Kwe, kwe, kwe. Kwe, kwe, kwe."

121 Tai huyo akatosheka, hakutaka kujipumbaza naye tena, kwa hiyo alifanya tu mruko mkubwa mno, namna *hiyo*, akapiga mbawa zake kama mara mbili, naye alikuwa juu ya mpaka wa ule msitu; aliweka tu mbawa zake, hakuzipigapiga tena, alitandaza tu mbawa zake. Na kila wakati upepo ungeingia,

angepanda juu zaidi. Upepo ungeingia, angepanda juu zaidi, bila kusogeza unyoya, alijua tu jinsi ya kuweka mbawa zake. Nikamtazama, nikaiangusha bunduki yangu, nikamtazama, akawa mdogo, mdogo, mpaka akatoweka.

122 Nikawazia, "Ee Mungu, ndivyo hivyo, ndivyo hivyo. Si jiunge na *hili*, na uchukue karatasi zako kutoka kwa *hili hapa*, jiunge na *hili*, jiunge na *hili*, jiunge na *lile*, pitia mstari mmoja wa maombi; Oral anapitia hapo, unapitia wake, na kupitia mwingine, kupitia mwingine. Si hivyo."

123 Ni kujua tu jinsi ya kuweka mbawa zako za imani katika nguvu za kufufuka Kwake. Na wakati Roho Mtakatifu anapoingia, panda juu yake, panda juu ya huyo kuchakulo anayeketi hapo, "Siku za miujiza zimepita. Hakuna kitu kama uponyaji wa Kiungu," kiumbe huyo asiyeweza kuondoka ardhini. Sisi ni tai. Haleluya! Roho Mtakatifu anaingia, nasi tunapanda kutoka kwenye njia ya hatari, moja kwa moja mpaka inafikia ambapo hata hatuyasikii tena.

124 "Siku za miujiza zimepita. Hakuna kitu kama uponyaji wa Kiungu. Ni telepathia ya kiakili. Kuna kasoro. Kanisa letu lingefanya *hivi*. Tuna lililo kubwa kuliko yote. Sisi ndio shirika kubwa zai-. . . " Panda tu juu yake.

125 Tandaza tu mabawa yako na useme, "Yesu Kristo, nakupenda, ninakuamini," sasa shikilia Kitabu hiki cha kale kilichobarikiwa chenye mabawa mawili *hapa* na uruke tu, haleluya, kwa maana Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele. Amina.

126 Mungu katika ulimwengu Wake! Je, mnaamini Yeye yuko katika ulimwengu Wake? Mwone katika ndege Wake, mwone kila mahali. Itatubidi kuondoka upesi kwenye somo hilo ili tupate hayo mengine; tunakaa mchana kutwa juu ya "Mungu Katika Ulimwengu Wake."

127 Sasa, hebu tumwone "Mungu Katika Neno Lake." Ni wangapi wanaoamini kwamba Mungu yuko katika ulimwengu Wake? Inua mkono wako. Vema. Mnaamini sasa Mungu yuko katika ulimwengu Wake. Sasa, tuchukue "Mungu Katika Neno Lake."

128 Sasa, Biblia ilisema, Yesu alisema, ya kwamba Neno lilikuwa ni Mbegu ambayo mpanzi alipanda. Hiyo ni kweli? Sasa, ninyi watu, hapa Oregon, mnapopanda mazao yenu, yanafanya nini? Haikubidi kwenda nje kila asubuhi, kuyachimbua. Kama ukipanda . . . ukipanda zao la mahindi, na kila asubuhi unatoka na kuyachimbua, uyaangalie, useme, "Vema, kwani . . . ? Sioni chochote kinachoendelea," halitakua kamwe. Huwezi—huwezi kulichimbua, inakupasa kulizika ardhini, hapo ndipo mahali pake; kila ukilichimbua unalichelewesha.

129 Nisikilizeni, nitasema jambo kubwa. Kila wakati unapoangalia dalili zako, unachelewesha uponyaji wako.

Usizichimbue tena, zimekabidhiwa Yeye aliyeahidi kuponya, Yeye anayewaponya hao wengine.

130 Unapopitia kwenye mstari wa maombi na kuwekewa mikono, Biblia ilisema, "Kuomba kwa imani kutamwokoa mgonjwa huyo," usiseme, "Vema, acha tuone kama ninajisikia vizuri zaidi, moyo wangu bora zaidi, mikono yangu . . . " usifanye hivyo, unaichelewesha, ikabidhi ardhini kwa sababu ni mbegu.

131 Je, mbegu hufanya nini? Angalia maskini—angalia maskini—maskini mtofaa huku nje. Nyinyi watu mnakuza matofaaa mengi. Angalieni, mtofaa mdogo wakati haupo zaidi ya, kile tunachoita huko mashariki, "chipukizi," mti mdogo *hivyo*. Je, mlijua ya kwamba kila tofaa, litakalowahi kuwa juu ya mti huo liko ndani yake wakati uo huo? Ikiwa sivyo, lilitoka wapi? Lilitoka wapi? Na mti huo wa tofaa ulio na . . . utakaokuzalia mamia ya mapishi ya matofaa, yanatoka wapi?

132 Unapoweka mmea huo mdogo huko nje, yapata namna *hiyo*, kutoka tu kwa mbegu ya tofaa, na kuuweka pale, na kila tofaa litakalowahi kuwa hapo juu, unalo ndani yake wakati huo, kwa uwezekano, kila pishi mia za matofaa utakayokusanya kutoka kwake, haiko urefu wa nusu inchi kwenda juu. Amina. Haya basi. Linatoka wapi? Liko ndani ya huo mtofaa wakati huo.

133 Nawe unapopandwa katika mauti Yake, kuzikwa, na kufufuka, kupandwa katika Kristo, na kupokea Uzima Wake wa Roho Mtakatifu ndani yako, kila kitu unachohitaji kote safarini kiko ndani yako wakati uo huo, kwa kuwa unakuwa Mbegu. Unaliona? Mungu katika Neno Lake.

134 Sasa, mti unapaswa kufanya nini? Unapoupanda, jambo pekee unalopaswa kufanya ni kuumwagilia maji, halafu hauna budi kunywa; majani yako ndani yake, matofaa yako ndani yake, ninii . . . kila kitu kiko moja kwa moja ndani ya mti huo, lakini unapaswa kunywa maji, hauna budi kunywa zaidi ya kipimo chake. Na unapokunywa, unasukuma nje, unasukuma majani nje, unasukuma maua nje, unasukuma nje matofaa; bali hauna budi kuendelea kunywa, kunywa, kunywa, upate kusukuma nje.

135 Nasi tunapochukua ahadi ya Mungu, na kuiingiza moyoni mwetu, tunaendelea kuimwagilia maji kwa imani, nayo inaendelea kusukuma nje, kusukuma nje. Haleluya! Kristo anapopandwa ndani ya moyo, Roho Mtakatifu, jambo pekee tunalofanya ni kunywa katika Neno hili la Mungu, Nalo linasukuma nje wokovu, linasukuma nje uponyaji wa Kiungu, linasukuma nje utukufu, linasukuma nje. Kila kitu tunachohitaji kiko moja kwa moja ndani yetu tunapopandwa katika Kristo Yesu.

136 Hii hapa tafsiri yangu juu Yake, kuhusu kuwa Maji: Yeye ni Chemchemi ya Uzima isiyokauka. Hutawahi kumwomba mengi kupita kiasi. Kamwe huwezi kumwamini kwa mambo

makubwa kupita kiasi, anapendezwa na wewe kumwaminia mambo makubwa, huwezi kumwaminia makubwa kupita kiasi.

137 Ungeweza kuwazia samaki mdogo yapata urefu wa nusu inchi, huko nje kabisa katikati ya bahari hiyo, akisema, "Sasa, ngoja kidogo, afadhali nifikirie jambo hili tena, afadhali ninywe kwa uangalifu maji haya kwa sababu huenda nikaishiwa mwaka huu." Vema, kama ungeweza kuelewa hilo, basi jaribu kuimaliza chemchemi ya wema wa Mungu kwako.

138 Je, unaweza kuwazia panya mdogo mwenye urefu wa nusu inchi hivi, chini yale maghala makubwa ya—ya—ya Misri, akisema, "Nitakula punje moja tu kwa siku, afadhali nijipimie punje moja kwa siku, kwa sababu huenda nikaishiwa kabla ya mazao mapya kuja." Loo, jamani. Anafanya nini? Anajinyima mwenyewe.

139 Hiyo ndiyo shida hasa ya kanisa siku hizi, katika kuchukua kanuni za imani za kanisa na mafundisho ya sharti na kujaribu kuyanyonya kutoka kwao, badala ya kulichukua Neno la Mungu, na kufurahia utimilifu wa ubatizo wa Roho Mtakatifu na mambo ya Mungu. Mbona? Neno Lake ni Mbegu, nalo Neno hili huzaa kwa jinsi Yake.

140 Sasa, ndio kwanza tupite uamsho mkuu, ulioenea nchini, kwa karibu miaka kumi na mitano. Tumevuna nini? Tulivuna lundo la wafuasi wapya. Naam. Kwa nini? Hiyo ndiyo aina ya mbegu tuliyopanda.

141 Kumbukeni, mvua hunyesha juu ya nchi kuinywesha, kuitayarisha, ambayo kwa ajili yake imetayarishwa. Na sasa, kumbukeni, kama ulikuwa na shamba la ngano hapa nje, nalo lilikuwa linakua, na masuke yake madogo yalikuwa yananing'inia juu ya . . . Unapoona kitu chochote kigumu sana, kinajifanya, suke zito lililojaa, sikuzote huinama. Natumaini mumepata hilo. Kwa hiyo sasa angalieni, sasa, lakini gugu dogo linalosimama pale, na ukame unaendelea, watu wanaombea mvua. Vema, maskini ngano hiyo inafanya, "Hah-ah, hah-ah." Kamwe haiwezi—kamwe haiwezi kuendelea tena, itakufa. Maskini hayo magugu yana furaha kupata maji tuseme. Mungu anatuma mvua, na mwajua nini? Mvua inaponyesha, maskini ngano hiyo hunyooka na kusema, "Utukufu kwa Mungu!" Inapaza tu sauti ya sifa za Mungu kwa sababu inapata uhai, nayo maji yayo hayo yanafanya magugu kukua, kufurahi vivyo hivyo, yanaweza kupiga mayowe kwa sauti kubwa vile vile.

142 Sasa, hivyo ndivyo Yesu alivyosema katika, mkitaka kulisoma, Waebrania mlango wa 6. Sina wakati wa kuingia katika hayo, maana unatuondokea, "Mvua hunyesha juu ya nchi mara kwa mara." Yesu alisema, "Mvua huwanyeshea wenye haki na wasio haki."

143 Tunaweza kuwaona watu wakipaza sauti, wakinena kwa lugha, wakicheza katika Roho, kila kitu namna hiyo, hiyo

haimaanishi, bado, wamempata. Loo, la. Niliona wengi wao wakifanya hivyo na hawakuwa naye lakini, "Kwa matunda yao mtawatambua," tunda, Roho Mtakatifu, kuliamini Neno la Mungu, na kulidhihirisha Neno la Mungu.

144 Hiyo inatupeleka kwenye wazo linalofuata, "Mungu Katika Mwanawe." Mnaamini Mungu yuko katika Neno Lake? Jinsi tungaliweza . . . *Hapa* nina Maandiko dazani moja yaliyoandikwa hapa kuhusu jinsi Mungu anavyojidhihirisha kupitia kwa Ibrahimu, kupitia watu mbalimbali namna hiyo, akithibitisha ya kwamba Yeye alikuwako. Lakini ili tusije . . . Ni wangapi wanaoamini kwamba Mungu yuko katika Neno Lake? Kwa kweli, Yeye ni Neno.

145 Sasa, "Mungu Katika Mwanawe." Mnaamini Mungu alikuwa ndani ya Mwanawe? Alikuwa ni dhihiri- . . . [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . . kasema, "Yachunguzeni Maandiko; kwa maana ndani Yake mnadhani mna Uzima wa Milele, Hayo Ndiyo yanayonishuhudia. Nisipozifanya kazi za Baba Yangu basi msiniamini." Ni mara ngapi juma hili tumepitia hilo, huku na huko, kuonyesha ya kwamba Yeye alikuwa Neno. Kwa hiyo mnaona maumbile, Neno, Mwana, yote yanaishia kwenye Mungu yeye yule, Mungu yeye yule akifanya kazi katika njia mbalimbali.

146 Yesu alikuwa Mungu aliyedhihirishwa katika mwili, Yeye alikuwa Mungu Neno. Kila mmoja wetu ataamini kwamba Mungu alikuwa ndani ya Kristo akiupatanisha ulimwengu kwa nafsi Yake. Yesu ni Mwana wa Mungu, huo ni mwili, naye Mungu alikuwa yule Roho aliyekaa katika hiyo maskani aliyojitengenezea Mwenyewe, mwili wa bikira. Mungu . . .

147 Hiyo ndiyo sababu Yeye alisema hapa, "Nimekuwapo pamoja nanyi siku hizi zote ninyi msinijue? Aliyeniona Mimi amemwona Baba." Kwa maneno mengine, "Mnamwona Baba akifanya kazi kupitia Kwangu. Mungu ni Roho; wale wamwabuduo Yeye imewapasa kumwabudu katika Roho na kweli." Mnaona? Mungu ni Roho. Na hapa tunaona Neno likidhihirishwa. Katika Yohana wa Kwanza tunaona, pia katika Yohana 11, inasema hapa kwamba . . . na pia katika Yohana 5:24, tunaona sehemu nyingi. Yohana 14, Yesu alisema kwamba, "Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi yeye naye atazifanya." Kwa nini? Ni Neno lililodhihirishwa ndani yao.

148 Hapa wakati fulani uliopita, nilikuwa nikihubiri, nikitukuza, naye mwanamke mmoja, ni mfuasi wa kanisa lingine . . . Sipendi kuyataja makanisa, madhehebu, majina, lakini mwanamke huyu, alikuwa mfuasi wa kanisa lililoamini katika uponyaji wa kiakili. Wanaamini kwamba—kwamba ibilisi ni wazo, na Mungu ni wazo, na mawazo ya—yako ni chochote yalicho. Wanakana Uungu wa Yesu Kristo. Katika siku hii

ambayo, wakati . . . Watu wanajaribu kumfanya Yesu kuwa ni mtu tu.

149 Mbona, Yeye alikuwa ni zaidi ya mwanadamu! Kama alikuwa mwanadamu tu, sote tumepotea. Alikuwa Mungu, si chochote pungufu ya Mungu, Yeye alikuwa ni Mungu aliyedhihirishwa katika mwili, Yehova, Baba, akiishi ndani ya Mwanawe, akiupatanisha ulimwengu kwa Nafsi Yake.

150 Hiyo ndiyo sababu tuliagizwa na Mathayo Mtakatifu pale, "Wabatizeni katika Jina la Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu." Ati nini? Sio Miungu watatu, madhihirisho matatu ya Mungu yeye yule. Mungu Baba alikuwa ni Nguzo ya Moto, alifanyika mwili na kukaa miongoni mwetu: Mungu Mwana. Mungu juu yetu, Mungu pamoja nasi, sasa Mungu yeye yule, Roho Mtakatifu ndani yetu. Ofisi tatu: Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu. Ni Mungu yeye yule, si Miungu watatu, yule Mungu mmoja akijifanyia Mwenyewe ofisi tatu, madhihirisho matatu. Amina.

Loo, ni u—ulimwengu wa jinsi gani tunaoishi! Angalieni, kikamilifu. Sasa, alipokuwa hapa duniani . . .

151 Mwanamke huyu alisema, "Bw. Branham," akasema, "Ninafurahia kukusikia ukizungumza, lakini kuna kosa moja ninalopata kwako."

Nami nikasema, "Ni lipi hilo?"

Akasema, "Unajivuna sana juu ya Yesu."

152 "Loo," nikasema, "ikiwa hilo ndilo kosa pekee nililo nalo, ha—hakika nakushukuru, mama, kama hilo pekee ndilo unaloona nimekosea." Nikasema, "Natumaini Mungu yuko hivyo nitakapokuja kukutana Naye, aone tu kujivuna juu ya Mwanawe kupita kiasi ndilo kosa pekee nililokuwa nalo."

Naye akasema, "Vema, ulisema kuwa wewe ni wa kimsingi. Ulizungumza tu kwa Biblia wala hukuweka chochote . . . "

Nikasema, "Hiyo ni kweli hasa." Ningali nasema hivyo.

Akasema, "Kama ninaweza kukuthibitishia, kwa Biblia yako mwenyewe, ya kwamba Yeye hakuwa wa Kiungu . . . ? Wewe siku zote unamfanya wa Kiungu."

153 Nikasema, "A—alikuwa . . . Kama hakuwa wa Kiungu, Yeye alikuwa ndiye mdanganyifu mkubwa zaidi ulimwengu uliopata kuwa naye, nasi sote tuko katika dhambi. Kama alikuwa tu mtu wa kawaida, basi mtu mwingine yeyote angeweza kufa, mmoja kwa ajili ya mwingine. Hawezi kuwa chochote pungufu ya Mungu." Kweli.

154 Wakati alipokuwa akipanda kwenda Kalvari, siku hiyo, hayo madoa mekundu kotini mwake, yote yaliingia kwenye moja, huku nyuki wa mauti akimwuma kila mahali, akivuma, "Nimempata sasa." Waliweka tu kitambaa usoni Mwake na kumpiga kichwani, mnajua Yeye angeweza kuyatambua

mawazo. Walisema, "Tuambie ni nani aliyekupiga nasi tutakuamini." Walimtemea mate usoni, wakang'oa konzi zima la ndevu.

155 Ibilisi akasema, "Nimempata sasa." Naye alipokuwa akipanda mlimani, alisema, "Huyo asingeweza kuwa ni Mungu," ibilisi alisema, "huyo hawezi kuwa Mungu, Yeye asingeweza kuvumilia kitu kama hicho."

156 Nami ninaweza kumwona anapopanda juu, maskini mwili Wake dhaifu ukianguka namna *hiyo* alipokuwa akiyumbayumba kilimani, nyuki huyo akivuma kumzunguka, sauti hiyo ya mauti moja kwa moja kwenye mishipa Yake, akijua baada ya muda mfupi atakuwa ameondoka, nyuki huyo akasema, "Nimempata sasa."

157 Huyo ibilisi akasema, "Endelea, mauti, mchukue. Ni hayo tu, yeye si kitu, yeye ni kama tu wengine wao, atakufa. Mchome pale pale chini, naye atakufa."

158 Lakini angalia, ndugu, nyuki anapouchoma mwiba wake ndani kabisa, hataung'oa mwiba tena, hatakuwa na mwiba mwingine, ataung'oa huo mwiba. Wakati uchungu wa mauti unapoweza kumjia mtu wa kawaida, kwa sababu alikuwa mwenye dhambi, angeweza kuung'oa mwiba huo na kumchoma mtu mwingine, lakini wakati huo yeye aliuchoma mwiba wake katika mwili wa Imanueli. Haleluya! Ikaung'oa huo mwiba kutoka kwa mauti.

159 Nyuki anaweza kuvuma na kupiga kelele za kila namna, maskini huyo...Na mdudu yeyote anayethubutu kuchoma ndani sana, hupoteza mwiba wake, nayo mauti yalipomchoma Mwana wa Mungu, yalipoteza mwiba wake. Si ajabu Paulo angeweza kusema, "Mauti, u wapi uchungu wako? Kaburi, u wapi ushindi wako?" Hakika. Alikuwa zaidi ya mwanadamu, Huyo alikuwa ni Imanueli, Mungu pamoja nasi.

160 Naye akasema, "Nitakuthibitishia, kwa Biblia yako, ya kwamba yeye hakuwa wa Kiungu."

Nikasema, "Hebu tusikie ukifanya hivyo."

Akasema, "Yohana Mtakatifu mlango wa 11, Biblia ilisema ya kwamba Yesu alipoenda kwenye kaburi la Lazaro 'Alilia.'"

Nami nikasema, "Je, hayo ndiyo Maandiko yako?"

Akasema, "Naam, asingeweza kuwa wa Kiungu na kulia."

161 Nikasema, "Mama, unajua nini? Hoja hiyo uliyo nayo ni nyembamba kuliko mchuzi uliotengenezwa kwa kivuli cha kuku aliyekufa kwa njaa." Nikasema, "Naam, huna na—nafasi kwa chochote hapo." Nikasema, "Unashindwa kuona Yeye alikuwa Mungu na Mwanadamu pia, alikuwa Mungu-Mtu, Mungu alikuwa ndani Yake." Hiyo ni kweli. Nikasema, "Hebu nikuulize jambo moja. Alishuka kaburini akilia, alikuwa ni Mwanadamu," analia pamoja na waliao; anahuzunika pamoja

na wenye huzuni; anafurahi pamoja na wale ambao, wamejaa furaha; "lakini aliposhuka kaburini, akisimama pale, maskini mabega Yake yameinama chini," Biblia ilisema, "Hakuna uzuri, hata tumtamani," "kasema, 'Ondoeni hilo jiwe,' akayanyosha maskini hayo mabega, 'Lazaro, njoo huku.' Naye mtu, aliyekuwa amekufa siku nne kaburini, ameoza, akawa hai na kusimama kwa miguu yake, huyo alikuwa ni zaidi ya mwanadamu." Amina. "Huyo alikuwa ni Mungu katika Mwanawe." Haleluya! Mwanadamu hawezi kufanya hilo.

162 Yeye. . . Nitakubali Yeye alikuwa Mwanadamu aliposhuka kutoka mlimani, usiku huo, alikuwa na njaa huko juu, akashuka, akitafuta chakula, akitafuta kote juu ya mti apate chakula. Alikuwa ni Mwanadamu alipokuwa na njaa, lakini alipotwaa biskuti tano na samaki wawili na kuwalisha watu elfu tano, huyo alikuwa ni zaidi ya mwanadamu, huyo alikuwa ni Mungu katika Mwanawe. Amini?

163 Yeye alikuwa Mwanadamu alipolala kule nje nyuma ya ile meli usiku huo, nayo ikapeperushwa huku na huku kama kifuniko cha chupa katika dhoruba, wakati pepo elfu kumi wa baharini walipoapa wangemzamisha. Alikuwa ni Mwanadamu amelala pale usingizi, mchovu, nguvu zilikuwa zimemtoka, alikuwa ni Mwanadamu, lakini alipoamshwa, akaenda kwenye demani ya hiyo mashua, akakanyaga kwa mguu Wake, akaangalia juu, akasema, "Amani, tulia," nao upepo na mawimbi vikamtii, huyo alikuwa ni zaidi ya mwanadamu, huyo alikuwa ni Mungu katika Mwanawe. Amina. Haleluya!

164 Alikuwa ni Mwanadamu akilia msalabani, "Naona kiu. Nipe maji ninywe." Lakini katika siku hiyo ya tatu wakati alipoivunja mihuri ya mauti, kuzimu, na kaburi, na kufufuka tena, alithibitisha Yeye alikuwa Mungu. Amina.

165 Mwanaume au mwanamke yeyote aliyewahi kufikia umuhimu wowote anaamini hivyo. Imeichangamsha mioyo ya washairi kwa miaka mingi. Kama ningaliweza kumwita jukwaani, leo, mtu fulani aliyeamini jambo hilo, namwazia Eddie Perronet. Nyote mnamjua mshairi huyo, Eddie Perronet. Hakuna mtu ambaye angenunua mashairi yake, hawakutaka kujihusisha nayo kwa vyovyote vile. Siku moja alikuwa analia, akaingia katika chumba chake cha kusomea, akasema, "Ee Mungu, nifanye nini?" Naye akashika kalamu yake, akaandika ule wimbo wa uzinduzi. Ati ulisema nini, Eddie Perronet? Akasema:

> Wote na wazisifu nguvu za Jina la Yesu!
> Malaika na wamsujudie;
> Leteni taji ya kifalme,
> Na kumtawaza kuwa Bwana wa wote; (Amina.)

Mwingine akasema:

Alipoishi, alinipenda; alipokufa, aliniokoa;
Alipozikwa, aliziondolea mbali dhambi zangu;
Alipofufuka, alinihesabia haki bure milele:
Siku moja yuaja—loo, siku tukufu. (Amina.)

Mungu katika Mwanawe, akiupatanisha ulimwengu kwa nafsi Yake. Amina.

Alipoishi, alinipenda; alipokufa, aliniokoa;
Alipozikwa, aliziondolea mbali dhambi zangu;
Alipofufuka, alinihesabia haki bure milele:
Na siku moja yuaja—loo, siku tukufu.

Hoskins aliandika:

Ninapoukagua msalaba wa ajabu
Ambapo Mfalme wa Utukufu alifia,
Ninahesabu umaarufu wangu wote kuwa hasara tupu,

Kipofu Fanny Crosby alipiga kelele:

Usinipite, Ee Mwokozi mpole,
Kisikie kilio changu kinyenyekevu;
Unapozuru wengine,
Usinipite.

Kwa maana Wewe, ni mkondo wa faraja yangu yote,
Zaidi ya uhai kwangu,
Ni nani niliye naye duniani mbali na Wewe?
Au ni nani mbinguni ila Wewe? (Amina. Amina.)

166 Mungu katika Mwanawe, mnaamini alikuwa? Alionekana kama Mungu, alitenda kama Mungu, alisema Yeye alikuwa Mungu, Alilia kama Mungu, aliponya kama Mungu, alikufa kama mwanadamu, kisha akafufuka kama Mungu. Alikuwa ni Mungu aliyedhihirishwa katika mwili, Mungu alikuwa ndani ya Mwanawe. Je, mnaamini hilo? Mungu alikuwa katika ulimwengu Wake. Mnaamini hilo? Mungu yuko katika Neno Lake. Mnaamini hilo? Mungu yuko ndani ya Mwanawe. Mnaamini hilo?

167 Je, mngeweza kumwona katika Kristo? Yesu alisema, "Unaponiona Mimi unamwona Baba. Kwa nini unasema, 'Unionyehe Baba'?" Mungu alikuwa ndani ya Mwana, akiupatanisha ulimwengu kwa nafsi Yake. Sasa, "Mungu Katika Ulimwengu Wake." Mnaamini hilo? "Mungu Katika Neno Lake." Mnaamini hilo? "Mungu Katika Mwanawe." Mnaamini hilo? Sasa "Mungu Katika Watu Wake." Amina.

168 Hapo unapata Baba, Mwana, Roho Mtakatifu, Mungu yeye yule wakati wote, akijidhili. Wakati mmoja akiwa mtakatifu, mwanadamu akiwa mbali Naye, asingeweza kumkaribia, hata kondoo akiugusa mlima, au ng'ombe, hana budi kuchomwa mkuki. Aliposimama juu ya Sinai na kupaza Sauti Yake, hakuna

kitu kingeweza kukaribia, kwa sababu hapakuwa na dhabihu ila mnyama; huyo alikuwa ni Mungu juu yetu.

169 Kisha Mungu akajidhili, akashuka chini nasi tukamgusa, Timotheo wa Kwanza 3:16, "Bila shaka siri ya utauwa ni kuu, kwa maana Mungu alidhihirishwa katika mwili, akaonekana na Malaika, akaaminiwa, akachukuliwa juu Utukufuni." Tulimwona Mungu akijidhihirisha Mwenyewe kupitia Mwanawe, Kristo Yesu.

170 Sasa, Mungu juu yetu, Mungu pamoja nasi, sasa Mungu ndani yetu. Yote ambayo Mungu alikuwa aliyamimina ndani ya Kristo, na yote aliyokuwa Kristo aliyamimina ndani ya Kanisa, "Bado kitambo kidogo, nao ulimwengu hautaniona tena; lakini ninyi mtaniona Mimi. Kwa kuwa Mimi," na *Mimi* ni kiwakilishi nafsi, "Mimi nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hata mwisho wa utimilifu." Haleluya! Utukufu! "Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele."

> Alipoishi, alinipenda; alipokufa, aliniokoa;
> Alipozikwa, aliziondolea mbali dhambi zangu;
> Alipofufuka, alinihesabia haki bure milele;

171 Si ajabu Yeye ni Shina na Mzao wa Daudi; Nyota ya Asubuhi; Yeye aliyekuwako, aliyeko, na atakayekuja; Yeye aliyekuwa amekufa yu hai hata milele, akijidhihirisha Mwenyewe baada ya miaka elfu mbili, inathibitisha ya kwamba Yeye yuko hapa. "Mungu Katika Ulimwengu Wake," "Mungu Katika Neno Lake," "Mungu Katika Mwanawe," "Mungu Katika watu Wake." "Yesu Kristo yeye yule jana, leo na hata milele."

172 "Utuonyeshe Baba yatutosha." Mungu katika watu Wake siku ya Pentekoste, Mungu katika Petro wakati kivuli chake kilipopita juu ya wagonjwa, kikawaponya, Mungu katika Paulo, hata walichukua kutoka mwili wake leso na nguo. Haleluya! Mungu yuko hapa, leo hii. Mnaamini hilo? Mungu, mnaamini Yuko katika ulimwengu Wake? Mnaamini Yuko katika Neno Lake? Mnaamini Yuko katika Mwanawe? Mnaamini Yuko katika watu Wake?

173 Tumelitazama juma hili, muda baada ya muda, kazi zile zile ambazo Mungu alizifanya kupitia Sulemani, ilikuwa ni Mungu, kazi zile zile alizofanya kupitia pale, alizifanya kupitia kwa Yesu, Mwanawe. Jambo lile lile tulilomwona akifanya kupitia Mwanawe, tunamwona akilifanya kupitia Kanisa Lake, ikimfanya Yeye yule jana, leo, na hata milele, "Mungu Katika Ulimwengu Wake," "Mungu Katika Neno Lake," "Mungu Katika Mwanawe," "Mungu katika watu Wake." Amina. Amina.

174 Na tuinamishe vichwa vyetu. Nitarudi, wakati mmoja, ninapoweza kuhubiri muda mrefu nitakavyo. Haleluya! Mnaamini hilo? "Utuonyeshe Baba, yatutosha. Utuonyeshe tu Baba, itatutosha."

175 Jinsi tunavyomshukuru Bwana kwamba anabaki kuwa Mungu! Kwa nini tusimshukuru kwa sababu a—alimtoa Mwanawe wa pekee, Mwanawe wa pekee, ili awalete wana wengi ulimwenguni, apate kujionyesha Mwenyewe kuwa hai leo! Yesu alikufa, Mwana pekee wa Mungu, ili atufanye sisi kuwa wana, apate kufanya mapenzi Yake kupitia sisi.

176 Tunapaswa kuona aibu jinsi gani, tukidai kuwa watoto wa Mungu na kumwacha ibilisi atusukume huku na huku kama afanyavyo! Tuna haki, tayari tumefufuka pamoja Naye. Mnasema, "Una nguvu?" La, bwana. Hatuna nguvu zozote, lakini tunayo mamlaka. Kuna tofauti kubwa kati ya nguvu na mamlaka. Kristo ana nguvu.

177 Mtu fulani aliniuliza muda mfupi uliopita, ndugu wa thamani, alikutana nami barabarani, akasema, "Ndugu Branham, wewe ni wa Jina la Yesu?"

Nikasema, "Mimi ni mtumishi wa Yesu." Mimi ni mtumishi Wake.

178 Angalieni, nataka kuwauliza jambo fulani. Anabaki yeye yule jana, leo, na hata milele. Je, ungependa Yeye awe Mwokozi wako, alasiri ya leo? Je, ungependa kujua kwamba Mungu huyu, aliye karibu, anaweza kuwa Mwokozi wako? Kama ungetaka, inua mkono wako, useme, "Ninataka kumkubali, Ndugu Branham, papa hapa nilipo, nitaamini." Mungu akubariki. Mungu akubariki. Hilo ni jema. Mungu akubariki. Mungu akubariki. Mungu akubariki. Hilo ni jema. Juu kwenye roshani, kote kila mahali, Mungu awabariki. Hilo ni jema. Mikono kadhaa iliinuliwa.

179 Loo, mnaona, tunapopata tu joto ya mkutano sasa, mnaona jambo hilo, Shetani akijaribu kuwazuia? Ibilisi huyo wa kale! Aminini sasa hivi, hii ndiyo saa, huu ndio wakati, katika kanisa lako mwenyewe, unaweza kuanzisha uamsho na kufanya kazi za Mungu. Yesu alisema, "Yeye aniaminiye Mimi . . . Yeye ambaye . . . Yeye aliyetumwa na Mungu hufanya kazi za Mungu." Amina. Aminini sasa. Msilitilie shaka. Aminini, msiwe na shaka. Iweni na uchaji sana kwa dakika moja tu na mwombe.

Je, wewe . . . ? Kimya kabisa sasa.

[Dada mmoja ananena kwa lugha na ndugu mmoja anafasiri—Mh.] Shh, shh, shh, shh!

180 Amina. Mungu ashukuriwe. Sisi sote tunaamini, na tunaamini katika kunena kwa lugha na kufasiriwa kwa lugha. Tunaamini ya kwamba Mungu hufanya hivyo, Naye hufanya hivyo ili kulijenga Kanisa Lake. Sasa, kama niliuona huo ujumbe vizuri, ulisema kitu kuhusu "Aminini kwamba Bwana angejidhihirisha Mwenyewe na kufanya jambo fulani katika . . . kwa ajili ya watu Wake."

181 Sasa, papo hapo unapoketi, kabla hatujaitisha mstari wa maombi, ninataka kuwaulizeni jambo fulani. Kila nafsi iliyomkubali Kristo, mtafanya ahadi hii kwangu mimi na kwa Mungu, Mungu kwanza halafu mimi, kwamba kila mtu hapa, anayemwamini Bwana Yesu Kristo, ataenda kwenye mojawapo ya makanisa haya mazuri hapa, na kuomba ubatizo wa Kikristo, ikiwa bado hujabatizwa kwa maji, na ukae hapo, hata utakapompokea Roho Mtakatifu, na—nawe utayatoa maisha yako kwa Kristo kwa ajili ya huduma? Yeye . . . "Wote walioamini waliongezwa kwa Kanisa." Je, hiyo ni kweli?

182 Ni wangapi wataahidi jambo hilo, ambao hawajawahi kufanya hivyo, watamwahidi Mungu, sasa hivi, kwa neema Yake, utafanya hivyo? Kama unaweza kumwona Mungu akijidhihirisha Mwenyewe miongoni mwa watu Wake, alasiri ya leo, inua mkono wako, useme, "Nitafanya hivyo." Mungu akubariki. Inua mkono wako, sema tu, "Mimi . . . " Mungu akubariki. Mwingine, Mungu akubariki. Wewe, wewe, wewe, wewe. Angalieni tu hiyo mikono.

183 Yote hapa chini, kwenye orofa ya chini sasa. Ni wangapi, wasema, "Kama ninaweza kumwona Mungu akijidhihirisha Mwenyewe na kujithibitisha Mwenyewe papa hapa miongoni mwa watu Wake, nilimwona katika ulimwengu Wake, ninaamini Yeye yuko katika Neno Lake, na katika Mwanawe, na Mwanawe ni yeye yule jana, na hata milele, iwapo ninaweza kumwona Mwana akianza *kutenda* mambo, kufanya jambo lile lile alilofanya alipokuwa hapa duniani, nitaamini hilo kwa moyo wangu wote, na nitafanya maungamo, niende kanisani na nibatizwe, na kuliitia Jina la Bwana"?

184 Kwenye roshani hapa, mkono wangu wa kushoto, je, ningeweza kuona mikono pale? Sema, "Namwahidi Mungu hilo." Je, yeyote kati yenu hangeweza kupatana kuhusu hilo, ambaye si Mkristo? Kwa njia hii inueni mikono yenu ili niweze kuwaona. Na Mungu aweze kuwaona, atajua, Yeye anaujua moyo wako. Kurudi kwenye roshani upande huu, siwezi kuona huko nyuma, kuna giza sana, lakini inueni mikono yenu kwa Mungu na kusema, "Nitafanya. Nitafanya." Ninaweza kuona kupepea au kitu kama hicho, siwezi kujua ni kipi.

185 Huko nyuma upande huu, inua mkono wako, ninaamini wewe ni mwaminifu, utafanya hivyo. Inua mkono wako. Mungu akubariki. Pande zote. Kuna wengine hapa sakafuni sasa? Hapa chini, sema, "Nitamwinulia Mungu mkono wangu." Mungu akubariki, Mama. Mungu akubariki hapa, Bwana. Hilo ni zuri sana, sana.

186 Mtu mwingine? Mimi . . . Mungu anaujua moyo wako, wewe maanisha hivyo, sawa. Usisubiri zaidi. Usiku wa leo, nenda kwenye mojawapo ya makanisa haya hapa, papa hapa mahali

fulani, na...kubatizwa, kuliitia Jina la Bwana kwa sababu, kumbuka...

187 Je, unaamini kwamba mimi ni mtumishi Wake? Inua mkono wako. Useme, ikiwa nimepata neema machoni pako juma hili, inueni mikono yenu, kila anayetaka kuwa mwaminifu na kusema, "Kweli ninaamini, Ndugu Branham." Sikiliza, kuja kwa Bwana kumekaribia kuliko unavyodhania. Sijafundisha fundisho hapa, ni kukaa tu moja kwa moja na Ujumbe wa siku hizi.

188 Kumbukeni ishara ya mwisho ya Ibrahimu. Pia mnakumbuka ni Nani aliyeshuka kwenda kule? Ishara ya mwisho ya Ibrahimu? Angalia jambo lile lile hapa katika wakati wa Wayahudi, wakati walipokataliwa, hili hapa mwishoni mwa wakati wa Mataifa.

189 Kama nilivyowaambia juma hili lote, na kulielezea kwa makini, na kuwathibitishia, kuhusu kwamba kamwe katika historia hatujawahi kuwa na mwinjilisti hudumani...Sankey, Moody, Knox, Calvin, kwa lile kanisa baridi la kawaida, huko nje, yale makanisa ya Lutu, huko nje Sodoma, kamwe hawakumpokea Roho Mtakatifu na kuzaliwa na kutoka ndani yake. Lakini huko nje tuna mjumbe wa ajabu, huko nje siku hizi, kwa jina la Billy Graham, G-r-a-h-a-m, kama Abraham. Mnalipata?

190 Kuna Kanisa lililoteuliwa. Kuna...Angalia ni ujumbe wa aina gani ulioshuka kule na kuwahubiria, "Tokeni, tokeni, tokeni, tokeni." Lakini Mtu huyu alifanya nini *hapa* juu? Aliwaonyesha tu ishara huku mgongo Wake umeelekezwa kwenye hema. Mnaona? Hilo lilikuwa ni Kanisa teule.

191 Loo, msilale, marafiki, "Basi, amkeni enyi watakatifu wa Bwana, kwa nini kusinzia wakati mwisho unakaribia, lakini iweni tayari kwa ajili ya wito huo wa mwisho," nao huo wito unaendelea. Iweni na imani.

192 Baba wa Mbinguni, mimi ni mtumishi Wako, na—naikabidhi ibada hii Kwako. Nimehubiri Neno Lako vizuri zaidi nijuavyo, muda huo mfupi, kwa wasiwasi, na uchovu, na kudhoofika. Bwana, watu wamehudhuria, usiku baada ya usiku wamerudi kana kwamba wa—walitaka kusikiliza zaidi.

193 Sasa, Mungu, ninaomba ya kwamba kila mtu uliyemwita, watakuja kwenye mkutano huu. Tujalie, Baba. Naomba makanisa haya yajazwe na hawa watu. Jalia waje wakiungama dhambi zao na kubatizwa, wampokee Roho Mtakatifu. Tujalie, Bwana.

194 Weka ninii Yako...Hawa wanaokaa hapa sasa, ambao wako njiani kuelekea kwenye nchi ya ahadi, hawajidai kuwa wa ulimwengu huu, sisi ni wasafiri na wageni. Tumekiri kwamba tunatoka katika Ufalme mwingine, tulikufa katika ufalme wa kale na tumefufuliwa pamoja na Mfalme wetu. Yeye ni Roho,

anayeishi miongoni mwetu, akifanya kazi, Uhai Wake ndani yetu, akitupa sisi mamlaka ya kuhubiri Neno Lake na, akiishi kupitia kwetu, anafanya miujiza Yake Mwenyewe anapokwenda, akidai na kuonyesha ya kwamba asili ya Roho Wake, alipokuwa hapa duniani, ingali ni jambo lile lile leo. "Mungu Katika Watu Wake." Utubariki sasa.

195 Wewe utaninii. . .Ingekuwa ni juu Yako, Baba, kufanya yaliyosalia; nimehubiri, nikatoa wito wa madhabahuni, mikono imeinuliwa, niliwaaminisha Kwako. Mungu, jalia kwamba watakuwa tuzo za huu mkutano, hawatasahau kamwe, kila mahali wanapoangalia, wataweza kumwona Mungu, kila mahali. Lijalie. Tubariki pamoja sasa.

196 Sasa, tunangojea kukuona ukiingia ndani, Baba, kwenye wimbi. Njoo, kama vile Wewe ulivyofanya usiku ule kwenye maskini ile meli iliyotaabika, ambapo matumaini yote yalikuwa yametoweka ya kwamba wangeweza kuokolewa. Watu walikuogopa, Naye akasema: "Msiogope; ni Mimi; mwe na moyo wa ushujaa."

197 Mungu, jalia leo, ili watu wapate kujua, ambao wamekukiri Wewe kama Mwokozi wao, kwamba hawana haja ya kuhofu, Wewe uko hapa, yeye yule jana, leo, na hata milele, Mungu katika watu Wake. Tujalie, Baba, kupitia Jina la Yesu. Amina.

198 Ni wangapi wenu mlio na kadi za maombi sasa? Inueni mikono yenu. Je, kuna wowote hapa wasio na kadi za maombi (Inua mkono wako.) na bado ni wagonjwa? Loo, jamani. Vema, hukupata hata theluthi moja yao. Nilimwambia Billy awasambazie hao kadi za maombi. Vema, ninyi msio na kadi za maombi, inua mkono wako tena, hebu nione mlipo. Hmm, kila mahali tu. Sawa, niangalieni mimi.

199 Nilisema jambo fulani jana usiku ambalo sikupaswa kusema. Nililisema upesi, kisha nikalishika tena. Nilisema, "Watu wa Marekani hawaukubali upambanuzi." Hawaukubali, kama wanavyofanya huko ng'ambo, bila shaka sivyo, uamsho unaendelea huko bado. Lakini nilisema, "Mpaka Mungu atakaponiongoza tena, sitatumia upambanuzi. Baada ya miamsho hii kumalizika, nitaacha. Nikija tena, nitakuwa nikiwaombea wagonjwa." Lakini, hivi mliona, niliweka, "*Kama* Bwana akiniongoza"? Maana siwezi kuidhibiti, Yeye hufanya udhibiti, mimi ni chombo tu.

200 Kama vile tu maikrofoni hii, mnanisikia kupitia maikrofoni hii, maikrofoni siyo mnayoisikia, ni mimi. Nayo . . . Mimi ni bubu tu. Hiyo maikrofoni bila kelele kupiga kioo hicho itakuwa ni bubu. Vivyo hivyo mimi ni bubu kwa mambo haya, isipokuwa Mungu anene kupitia kwangu. Mnaamini hilo? Je, aliahidi katika siku za mwisho angefanya mambo haya? Tunajua hilo. Ile sehemu ndogo tu ya muda ambayo tumeona wiki hii, tunaamini.

201 Mtu fulani katika sehemu hii, asiye na kadi ya maombi, inua mkono wako tena na uombe. Mungu alijalie. Huyu mama, anayeketi mwisho hapa, akiniangalia, niliona ulikuwa umeinua mkono wako, hukuwa na kadi ya maombi. Sasa, uko karibu na mimi, ili Roho aanze.

202 Je, unaniamini mimi kuwa ni nabii Wake, ama, mtumishi Wake? Unaamini hilo? Kwa moyo wako wote? Ikiwa Mungu atanifunulia shida yako, utaniamini basi? Jua . . . Unajua kama ni kweli au la. Ulikuwa na vidonda vinavyotoka damu. Umefanyiwa upasuaji kwa ajili yake, una wasiwasi. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako. Inua mkono wako ikiwa hiyo ni kweli. Aligusa nini? Nitamtaka huyu mama asimame. Simama kwa dakika moja tu, Mama.

203 Ili huyu mama aweze kujua, nataka kumwuliza swali. Huyo hapo ameketi hapo, hana kadi ya maombi, hakuna chochote, ni mwanamke tu aliyeingia, akaketi chini. Lakini alikuwa ameketi pale kwa imani, kwa maana yuko katika hali mbaya. Kila ulichoambiwa ni kweli. Hiyo ni kweli, Mama? Inua mkono wako, kama yale yaliyosemwa, juu ya tatizo lolote ulilokuwa nalo, inua mkono wako. Wewe. Hii . . . Naam, hiyo ni kweli. Mungu akubariki. Vema.

204 Sasa, simjui huyu mama, hii hapa Biblia, sijawahi kumwona maishani mwangu, yeye ananizidi umri, tulizaliwa tukiachana kwa miaka kadhaa, umbali wa maili nyingi, mara ya kwanza kukutana. Lakini alifanya nini? Alikuwa akiombea jambo fulani, naye akamgusa Kuhani Mkuu, na mara alipomgusa, Yeye alinigusa papa hapa na kumwambia. Sasa, usiwe na wasiwasi tena, utapata afya, imani yako imekuokoa. Amina.

205 Ni wangapi wataamini sasa, Mungu yuko ndani ya watu Wake? Mnaamini? Huyu hapa mwanamke ameketi, papa hapa, akiwa na wasiwasi, anashangaa, ugonjwa wa kansa anaohofia. Amini kwa moyo wako wote, usiwe na shaka, kuwa tu na imani, Amini kwamba Mwana wa Mungu anakuponya, na unaweza kwenda nyumbani na kuwa mzima. Unaamini? Binti Staub, hilo ndilo jina lako. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako. Hatufahamiani, lakinini Yesu Kristo anakujua; kusudi tu usiukose. Unajisikia vizuri sasa? Acha kuhangaika, yote yamekwisha. Imani yako inakuponya.

206 Huyo hapo ameketi mwanaume, ameketi papa hapa kwenye safu, ameketi moja kwa moja hapo nyuma. Mtu huyo anasumbuliwa na ngiri. Yeye ni mgeni. Je, unayo kadi ya maombi? Huna. Huihitaji, ikiwa utaamini kwa moyo wako wote. Kama hatufahamiani, inua mkono wako. Vema. Wewe ni mwanamume tu, uliingia, ukaketi chini. Je, hiyo ni kweli? Lakini una haja ya kuponywa hii ngiri. Vema. Ikiwa unaamini kwa moyo wako wote, unaweza kuwa nayo. Amina.

207 "Mungu Katika Watu Wake," "Mungu Katika Ulimwengu Wake," "Mungu Katika Mwanawe," "Mungu Katika Watu Wake." Mnaamini? Hebu niwaonyeshe kitu ambacho huenda msininii . . . huenda msijue. Huyu hapa mwanamke ameketi, ameketi papa hapa, akinitazama. Anataka kufanya yaliyo mema, anajaribu kufanya yaliyo mema. Ana tabia ya kuvuta sigara, anajaribu kuziacha. Hiyo ni kweli. Ikiwa utaninii . . . Hiyo ni kweli, Mama? Usione aibu. Simama kwa miguu yako kwa dakika moja. Hatufahamiani. Je, una kadi ya maombi? Huna; huhitaji yoyote, wewe niamini. Katika Jina la Yesu Kristo, ninamlaani ibilisi huyo! Naomba usitamani nyingine. Nenda ukapone katika Jina la Yesu Kristo.

Ninakuomba umwamini Bwana Yesu Kristo. Unamwamini?

208 Mama anayeketi hapo nyuma, shinikizo kuu la damu, shida ya moyo. Kama utaamini kwa moyo wako wote, Mama, Mungu atakuponya. Mungu akubariki. Nenda nyumbani, uwe mzima. Mungu anakuponya. Je, unaamini hilo? Usiwe na shaka.

209 Mama anayeketi papa hapa akinitazama. Haleluya! Anateseka, anashangaa kuna shida gani. Ana kansa, pia ana kivimbe ama uvimbe anaosumbuka nao. Loo, natumai hataukosa. Mungu akurehemu. Bibi Knorr, amini kwa moyo wako wote. Amina. Hatufahamiani, sijawahi kumwona maishani mwangu. Kama hatufahamiani inua mkono wako, Mama. Umesimama hapo, ukiomba, unajua huna budi kufa kama jambo fulani halitatukia. Usiogope; hutakufa. Mwamini Bwana Yesu Kristo nawe utaishi.

210 "Mungu Katika Ulimwengu Wake," "Mungu Katika Neno Lake," "Mungu Katika Mwanawe," "Mungu Katika Watu Wake!" Je, mnaamini hivyo? "Yesu Kristo yeye yule jana, leo na hata milele." Inasambaa kwa kusanyiko zima. Je, unaamini kwa moyo wako wote sasa?

211 Ni wangapi wenu mnaoamini wachungaji wenu, huko nje, kuwa ni mtu wa Mungu? Inueni mikono yenu, kama mnawaamini wachungaji wenu. Mnapaswa kuwaamini, yeye ni sawa tu, kama . . . kuwaombea wagonjwa kama mimi. Ndugu, shukeni moja kwa moja hapa chini pamoja nami, ninawataka, mwombe pamoja nami, na kwa ajili ya watu hawa pia. Njoni moja kwa moja hapa chini. Njoo hapa, Roy, chukua *hii*.

212 Nataka kila mtu, katika mstari huu hapa, walio na kadi za maombi, asimame upande huu, papa hapa. Simama papa hapa, kila mtu. Biblia inasema nini? "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio. Wakiweka mikono juu ya wagonjwa, watapata afya." Je, mnaamini hilo? Je, mnaamini kwamba mimi ni mwaminio? Semeni, "Amina." Je, mnaamini kuwa mchungaji wenu ni mwaminio? Semeni, "Amina." Vema.

213 Sasa, tutawaita safu kwa safu, sehemu kwa sehemu; sehemu ile kwanza, sehemu hii ifuate, ile ifuate, ile ifuate. Msije kwa njia

zote mbili, mtachanganyikiwa kabisa huko juu, wala hamtaweza ku—kuninii . . . Msikilizeni Ndugu Roy, hapa, sasa.

214 Na wachungaji, ni wachungaji wangapi zaidi waaminio waliopo hapa, ambao kweli wanaiamini Injili, wachungaji wa Injili yote, wanaweza . . . mnaweza mkawa wageni, mngependa kuja na kusimama nasi ndugu? Hatumtengi mtu yeyote. Tunaamini ikiwa wewe ni mwaminio wa Kristo . . . Hiyo ni kweli, ndugu yangu? Hiyo ni kweli, ndugu yangu?

215 Kama mchungaji wako yuko hapa, unaamini katika kuwaombea wagonjwa, haijalishi . . . Ikiwa wewe unamwamini Kristo na unaamini kuwa hii ni ya Kristo, njoo hapa na upange mstari hapa, na ufanye wajibu wako, kama mtu wa Mungu, kusimama hapa na kunisaidia kuwaombea wagonjwa na wanaoteseka. Njoni huku, wachungaji.

216 Pangeni mistari miwili hapa. Nitashuka pamoja nanyi huko, katika muda mfupi tu, tutamwombea kila mgonjwa. Sitaki kusimama na kuzungumza kwa muda mrefu, nataka mpitie huku wakati upako huu ungali juu yangu. Unaamini sasa kwa moyo wako wote? Njoni papa hapa juu, wachungaji, nusu . . . baadhi yenu njoni huku. Ingieni moja kwa moja katikati ya hawa, papa hapa, na mfanye mistari miwili. Hiyo ni sawa. Mungu awabariki. Vema. Hebu tuimbe wimbo huu tena, sote pamoja:

> Amini tu, amini tu,
> Sasa, mambo yote yanawezekana, amini tu;
> Amini tu . . .

217 Sasa, mstari utakuwa unatoka huku, jamani. Mnaweza kuleta hicho kiti cha magurudumu, kipitisheni huku kwingine, maana i—itabidi kipitie huku, mtavuruga yote.

> Mambo yote yanawezekana . . .

Sasa hebu na tuinamishe vichwa vyetu, tufunge macho yetu, tuinue mikono yetu.

> Bwana, naamini,

Kila mtu sasa. Mheshimu Yeye . . . ? . . .

> Mambo yote yanawezekana . . .

[Ndugu Roy Borders anaendelea kuimba, kisha anaanza kuuelekeza mstari wa maombi. Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

> . . . naamini, Bwana, naamini,
> Mambo yote yawezekana, Bwana, naamini.

218 Kwa moyo wangu wote, ninaamini. Nadhani mlishangaa, wengi wenu, kwa nini ningetoka mwisho mmoja wa safu hadi mwingine, na wengi wenu mliniona nikishika mkono wako kwa wangu. Je, mliona hilo? Ni wangapi waliona hilo? Inueni mikono yenu. Nilikuwa nikiangalia kilichokuwa kinaendelea

baada ya hao wahudumu kuwawekea wagonjwa mikono. Nami nitasema hivi, kwa moyo wangu wote, kwamba angalau asilimia themanini wao waliponywa kabla hata hawajafika mahali nilipokuwa. Hakukuwa na mtetemo juu yao hata kidogo. Hiyo ni kweli kabisa. Hiyo ndiyo sababu yangu ya kuliangalia. Wachungaji wenu wana imani, jamani, waaminini tu.

219 Ninawapenda. Ninaamini ninyi ni watoto wa Mungu. Niombeeni, nitawaombea, na ninatumaini tutakutana tena. Hadi wakati huo, "Mpaka twonane." "Mpaka twonane tena." Kila mtu, pamoja sasa. Unampenda Bwana, moyo wako wote? Sawa. Sote pamoja sasa. Nitawaombea, ninyi niombeeni. Vema.

> Hata twonane! hata twonane!
> Hata twonane miguuni pa Yesu;
> . . . twonane! hata twonane!
> Mungu awe nanyi hata twonane tena!

220 Hebu na tuinamishe vichwa vyetu sasa, huku muziki huo mzuri . . . Wazieni nyakati nzuri ambazo tumekuwa nazo. Wana Maonyesho ya Ulimwengu yanayoendelea hapa, ambapo ulimwengu mzima unaonyesha mafanikio yake ya kisayansi. Lakini Kanisa linatambua ya kwamba, papa hapa, Mungu ana Maonyesho ya Ulimwengu, akionyesha mafanikio Yake, yale ambayo ameweza kufanya na Kanisa Lake.

221 Nimefurahia kila dakika ya . . . kila dakika. Ninakuja kwenu nimechoka, kama kawaida, lakini nitawaona tena siku moja. Mungu awabariki sasa. Tunapouvumisha wimbo huo pamoja, ombeaneni kidogo, hata tutakapoonana.

> Mungu awe nanyi hata twonane tena. (. . . ? . . .)
> Hata twonane! hata . . .

222 Bwana Mungu, uwe pamoja nao na uwasaidie, hata twonane, Baba, sasa, kupitia Jina la Yesu, kwa ajili ya utukufu wa Mungu.

Utuonyeshe Baba Yatutosha SWA62-0722
(Show Us The Father And It Will Suffice Us)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza Jumapili alasiri, tarehe 22 Julai, 1962, kwenye Kiwanda cha Silaha cha Taifa huko Salem, Oregon, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2023 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org